Nipashe
Ijumaa Juni 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580979
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 253,545,950
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Siku** ya Mtoto na sababu 10 ulawiti kukithiri

UKURASA 3



**PEREZ AMSHUKIA MBAPPE**

UKURASA 21



Wananchi wakiangalia basi la Zuberi lenye namba za usajili T435 DJS, baada ya kupata ajali katika eneo la Mwigumbi wilayani Kishapu mkoani Shinyanga juzi na kusababisha watu watano kupoteza maisha na wengine 26 kujeruhiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RPC: Dereva alifariki kabla basi kupinduka

• **Aliendesha** akiwa mgonjwa, watano wafa, 26 wajeruhiwa...



*Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 3

## CHONGOLO AGEUKIA MAKATIBU WAKE

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameonya...

## Fundi jokofu asakwa tuhuma mauaji ya mke wake

UKURASA 2



Mapadri wa Kanisa Katoliki wa Parokia mbalimbali za ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya, wakishiriki kushusha kaburini jeneza lenye mwili wa Padri Michael Samson ambaye aliuawa mwishoni mwa wiki na watu wasiojulikana, wakati wa mazishi yake kwenye makaburi ya Kanisa la Hija la Bikira Maria wa Fatima Mwanjelwa jijini Mbeya jana. **Habari uk. 2. PICHA: GRACE MWAKALINGA**



## ACT yataka CAG akague pato la tozo miamala simu

UKURASA 4

**MICHEZO** **NABI ATOA UBINGWA KWA FAMILIA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# RPC: Dereva alifariki kabla basi kupinduka

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DEREVA wa basi la kampuni ya Zuberi, Hamza Haule, amedaiwa kuugua na kufariki dunia akiwa kwenye usukani kabla basi hilo halijaanguka na kusababisha vifo na majeruhi.

Basi hilo lenye namba za usajili T435 DJS lilianguka juzi alasiri baada ya kugonga kingo za daraja eneo la Mwigumbi wilayani Kishapu mkoani Shinyanga na kusababisha watu watano kupoteza maisha na wengine 26 kujeruhiwa.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alisema jana kuwa kwa taarifa za awali chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa basi hilo kupata tatizo la kiafya na kufariki dunia akiwa kwenye usukani.

Alisema kuwa kwa mujibu wa taarifa ambazo jeshi hilo lilizipata na linaendelea na uchunguzi ili kubaini ukweli, zinadai kuwa dereva huyo kabla ya kuanza safari kutoka Mwanza kwenda Kahama, hakuwa vizuri kiafya na alipofika eneo hilo la Mwigumbi, alifariki dunia akiwa kwenye usukani.

"Ajali hii imegharimu maisha ya watu watano, watu wawili wamefia hapo hapo kwenye eneo la tukio, na watu watatu walifia hospitalini.

"Ninatoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto wawe wanachunguza afya zao kabla ya kuanza safari na endapo wakiwa hawajisikii vizuri, wasiendelee na safari ili kuepusha ajali zisizo za lazima," alisema.

Baadhi ya majeruhi wa ajali hiyo, akiwamo Daniel Sewe, walisema walipofika kwenye eneo hilo la Mwigumbi, basi lilipiga tuta na kuanza kuyumba kisha kupoteza uelekeo na kugonga kingo za daraja, likapaa juu na kuanguka.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kolandoto, Dk. Masunga Maneno, alisema hadi sasa watu walipoteza maisha katika ajali hiyo ni watano - watu wazima wanne na mtoto mmoja na walipokea majeruhi 26. Kati yao, 13 walitibiwa na kuruhusiwa.

Katika ajali hiyo, miongoni mwa waliofariki dunia ni mwalimu wa Shule ya Msingi Ng'hama iliyoko Mwalukwa wilayani Shinyanga, Kassam Kassam, huku Mwalimu Mashaka Kasomeko wa Shule ya Msingi Bulambila wilayani humo, akivunjika mkono wa kushoto. Walimu hao walikuwa wakitoka Mwanza walipokwenda kushiriki semina ya elimu jumuishi.

Watu wengine wanne ambao wamefariki dunia katika ajali hiyo, bado hawajatambuliwa majina yao na miili yao iko kwenye chumba cha kuhifadhi maiti katika Hospitali ya Kolandoto.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo (wapili kulia), akionyesha kwa waandishi wa habari jana, baadhi ya vifaa vya magari, vilivyokamatwa katika msako wa jeshi hilo, mkoani humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Padri aliyeuawa Mbeya azikwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VILIO na majonzi vimetawala katika Kanisa la Katoliki la Hija la Bikira Maria wa Fatima jijini Mbeya wakati wa mazishi ya Padri wa Kanisa hilo, Michael Samson (63) wa Shirika la Wamissionari wa Afrika (White Fathers) ambaye aliuawa mwishoni mwa wiki na watu wasiojulikana.

Padri huyo alitoweka kwenye Kituo cha Vijana wa Kanisa hilo (Youth Centre) kilichoko jijini Mbeya Juni 10, mwaka huu, baada ya kuaga kuwa alikuwa anakwenda kufanya mazoezi ya kutembea na hakurudi tena mpaka alipokutwa Juni 11 akiwa ameuawa.

Mwili wa Padri Michael ulikutwa umetupwa kwenye Mto Meta chini ya Daraja la Jakaranda ukiwa umechanganywa kwa kutenganishwa baadhi ya viungo na watu wasiojulikana kisha kuviringishwa kwenye blanketi.

Mazishi ya kiongozi huyo wa kiroho yalifanyika jana katika Kanisa hilo la Bikira Maria wa Fatima ambapo viongozi mbalimbali wa dini na serikali walishiriki wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, pamoja na Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Gervas Nyaisonga.

Kwenye mazishi hayo waombolezaji walionekana wakilia huku baadhi wakiligusa sanduku lililokuwa na mwili wake na baadhi ya waliokuwa wanaishi naye wakisema alikuwa mtu mpole na alikuwa anaongea na kila mtu.

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, ambaye Rais wa Baraza la Maaskofu Wakatoliki Tanzania, Gervas Nyaisonga, alisema walilipokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Padri Samson ambaye aliuawa kikatili na watu wasiojulikana.

Alisema kanisa linategemea kuwa wale wote waliohusika na tukio hilo watakamatwa na kuchukuliwa hatua ili liwe fundisho kwa watu wengine.

"Ni mwaka na nusu sasa tangu Padri Samson aje nchini Tanzania kuhudumu akitokea nchini Zambia, ni mambo ameyafanya katika kuhubiri na kutangaza neno la Mungu kifo chake kimetuumiza sana alisema," Askofu Nyaisonga.

Akimzungumzia wasifu wa marehemu, Katibu wa Shirika la Wamisionari Afrika Mashariki, Padri Anthony Alckias alisema waliishi vizuri na Padri Samson ambaye hakuwa na majivuno wala kiburi badala yake alimheshimu mkubwa na mdogo.

Mpwa wa Padri Samson kutoka Malawi, Enock Mawelera, alisema msiba huo umemsababishia msongo wa mawazo kutokana na mambo makubwa aliyomfanyia ikiwamo kumsomesha hadi kupata kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera, aliwaomba viongozi na waumini wa kanisa hilo kuendelea kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea kufuatilia na kuwakamata wale wote waliohusika na mauaji hayo.

# Fundi jokofu asakwa tuhuma za kuua mke

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa 396 kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya uhalifu, huku likimsaka fundi wa majokofu, Godbles Sawe (47), anayetuhumiwa kumuua mke wake.

Sawe, mkazi wa Kimara Suka mkoani Dar es Salaam, anatuhumiwa kumuua mke wake, Ester Gadau, kwa kumkata kichwani kwa kutumia kitu chenye ncha kali na kumsababishia umauti kisha kukimbia baada ya mauaji hayo.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alibainisha hayo jana jijini humo wakati akizungumza na waandishi wa habari huku akifafanua kuwa tukio hilo la mauaji lilitokea Jumanne ya wiki hii eneo la Kibamba wilayani Ubungo.

Kuhusu watuhumiwa 396, kamanda huyo alisema walikamatwa kupitia msako uliofanyika kwa kipindi cha mwezi mmoja kilichoanzia Mei 15, mwaka huu hadi Juni 15, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali mkoani hapo.

Alisema msako huo ulikuwa na lengo la kuzuia na kukabiliana na vitendo vya kihalifu vikiwamo unyang'anyi wa kutumia silaha, wizi wa magari na vipuri, wizi wa pikipiki, uvunjaji, dawa za kulevya na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Alisema katika tukio la unyang'anyi wa kutumia silaha, waliokamatwa ni Mohamed Bakari, maarufu Mremi, na wenzake 12 ambao wanatuhumiwa kupanga, kujihusisha na kutekeleza matukio mbalimbali yakiwamo ya kutumia silaha kama mapanga, nondo na visu.

Kamanda Muliro alisema kuwa kupitia falsafa ya ulinzi shirikishi, zimepatikana bastola mbili aina ya TAURUS Silver namba P-22 Cariba FL-22 LR iliyotengenezwa Miami nchini Marekani ikiwa na risasi mbili na ya pili ni aina ya Browning ikiwa na risasi 42.

Alisema kwa matukio ya uvunjaji, wamemkamata Omary Bwilani (34), mkazi wa Buza wilayani Temeke na wenzake 54 wakiwa na runinga nane zinazodaiwa kuwa ni za wizi zenye ukubwa tofauti.

"Watuhumiwa hao wamekutwa na sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) jozi tatu, buti jozi moja na kofia moja. Vingine ni DVD player moja na fedha Sh. 300,000 zilizoibwa," alisema.

Kamanda Muliro alisema katika msako huo wamewakamata watuhumiwa 15 wanaodaiwa kujihusisha na wizi wa magari na vipuri vyake.

"Tumewakuta na magari mawili, moja lenye namba za usajili T 617 DRU aina ya Suzuki Carry na lingine Toyota Wish jeusi ambalo limefutwa namba za usajili na kubadilishwa rangi kuwa jeupe, tumewakuta na vipuri mbalimbali vya magari na pikipiki.

"Vifaa walivyokutwa navyo ni mlango wa gari aina ya Toyota Prado, side mirror 38 za magari mbalimbali, namba za magari 47, gear box moja ya Toyota Hilux, taa za mbele 21 za magari mbalimbali na za nyumba zipatazo 14.

"Rim sita size 15 za magari madogo, exhaust pipe moja ya gari, kadi 26 za usajili wa magari na injini tatu za pikipiki wamekutwa na leseni moja ya biashara inayodhaniwa kuwa ni ya kughushi pamoja na mkataba wa mauziano ya gari ambao nao unachunguzwa," alisema.

Pia alisema watuhumiwa hao walihojiwa ili waonyeshe magari ya namba walizokutwa na kwamba mifumo ya kisheria inafuatwa kushughulikia tukio hilo.

Kamanda Muliro alisema wamekamatwa watuhumiwa 206 wakiwa na dawa za kulevya za aina mbalimbali zikiwamo heroine gramu 93, bangi kilo 222 na gramu 109 na mirungi kilo 3.5 ambao tayari wamefikishwa mahakamani.

Pia alisema mtuhumiwa Fatuma Juma, mkazi wa Tumbwi, Kigamboni na wenzake 80 wanatuhumiwa kukamatwa na pombe haramu ya gongo na wameshafikishwa mahakamani.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi limeweka mkazo wa kesi za ukatili wa kijinsia zipelekwe haraka na baadhi ya watuhumiwa waliofikishwa mahakamani ni Joshua Simangwe (66), mkazi wa Kipunguni Ukonga, anayetuhumiwa kuwalawiti wanafunzi watatu wenye umri wa chini ya miaka 18 wanaosoma huko Gongo la Mboto.

Alisema wanamshikilia Frank Barnabas kwa tuhuma za kujifanya askari na kufanya uhalifu wa kutapeli watu na kupita kwenye maduka, akidai anatafuta vipuri vya gari la polisi.

Alisema mtuhumiwa huyo amekuwa akishirikiana na mwenzake ambaye ni John Shija ambaye yeye anadaiwa kujifanya fundi wa magari ya polisi.




Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda, Biashara, Exaud Kigahe (kulia), akikabidhi ripoti na ramani shirikishi ya sensa za mashine za kusindika vyakula nchini kwa Mwakilishi Mkazi na Mkurungenzi wa shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) hapa nchini, Sarah Gordon-Gibson, baada ya kuizindua, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chongolo ageukia makatibu wake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameonya makundi ya uchaguzi ndani ya chama huku akipiga marufuku makatibu wa CCM kujipenyeza kugombea nafasi mbalimbali ndani ya jumuiya kwa kuwa ndiyo chanzo cha vurugu.

Chongolo alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha Baraza Kuu la Jumuiya ya Wazazi wa CCM.

Alisema katibu atakayechukua fomu kugombea kwenye jumuiya, jina lake litakatwa kwa kuwa baadhi yao ndiyo chanzo cha vurugu ndani ya nafasi wanazoshiriki.

"Wapo baadhi ya watendaji wangu wanasema 'unajua ukigombea kwenye jumuiya, hatuonekani au huku hakuna maneno'. Kama umeamua kuchukua mshahara wa CCM kwa dhamana ya kuwa mtendaji, kama umeamua kuwa mtendaji, kugombea nafasi ambazo zinakuletea mgongano wa maslahi ni marufuku," aliagiza.

Alieleza kuwa mtu akiamua kuwa mtendaji halafu utendaji wake una maslahi ya moja kwa moja na nafasi mbalimbali ambazo zikigombewa, inaleta shida, hivyo ni marufuku kugombea na kuahidi kulisimamia suala hilo.

"Mimi sipigi kelele, utaona nimekutoa nimekupeleka sehemu ukasubiri hatima yako, hatupo tayari kuwa na watendaji ambao wameamua kutukwamisha.

"Kinachonisikitisha ni nyie ambao mmenipa jukumu la kuwalipa mshahara na nimewapa jukumu la kuwakilisha kuwa wakurugenzi wa uchaguzi (makatibu) ngazi zenu na nyie mmeingia kwenye mifuko ya watu.

"Nisisitize ukiona mahali kelele zimekuwa nyingi, ujue umeondoka kwenye kutenda haki, umeamua kumbeba mtu mfukoni, tuache tabia ya kuwa wapiga debe wa wagombea," alionya.

Alisema jumuiya hiyo ni mwalimu wa jumuiya nyingine na kusisitiza kuwa inashangaza watu walioaminiwa, kufanya mambo ambayo yanakiuka kanuni na miiko ya chama.

"Unamkuta kiongozi unayemheshimu asubuhi yupo uchochoro huu, mchana ule na jioni mwingine, kinachosikitisha tumeingiza kampeni za nafasi ambazo muda wake haujafika, chama hiki kina utaratibu, kwenye chama chetu wala huhitaji kuweka wapelelezi wakubwa, bali wachunguzi ni wale wanaotaka nafasi moja," alisema.

Aliwaonya juu ya kutengeneza makundi ya uongozi kwa kuwa uongozi hutoka kwa Mungu.

"Tuache mambo hayo kwa kuwa ndiyo yanayovuruga utaratibu wa uchaguzi, mimi jukumu langu ni kusimamia katiba na siwezi kuwa na mgombea kwa kuwa ndiyo vitu vinavyoweza kumtengenezea mateso mtu.

"Ukiwa na mgombea, akikosa kwa miaka mitano unaishi unawaza, tuache kubeba watu, hii jumuiya inaonyesha aibu unapomkuta mtu anatembea na mgombea mfukoni," alisema.

Akizungumzia suala la ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, Chongolo alisema mmomonyoko wa maadili umekuwa mkubwa sana nchini na kwamba vitendo vya ovyo na ukatili wa kupindukia unafanywa kwenye jamii na kuitaka jumuiya hiyo kusaidia kupinga vitendo hivyo kwenye maeneo yao.

"Haitakuwa na tija kuitwa Katibu wa Malezi kwenye maeneo yetu halafu malezi yenyewe yanamomonyoka, ni heri tuue hayo majina mazuri mazuri ambayo hayaakisi kile ambacho jamii inafanyiwa.

"Lazima tubebe hilo jukumu kwa kuwa ni jukumu letu la dhati kuhakikisha sisi tunakuwa daraja la kusimamia na kutekeleza hili kwa vitendo.

"Ubakaji umekuwa sasa ni kama jambo la kawaida na mambo mengine mengi ya udhalilishaji wa kijinsia yameanza kuzoeleka, lazima tusimame kama jumuiya ya wazazi kukemea hili, na kukemea siyo unakemea halafu kesho unaonekana unamsubiri mwanafunzi wa shule au umeshikiria mkono wa binti ambaye yupo sawa na uliyemwacha nyumbani," alisema.

Kuhusu uwekezaji ndani ya jumuiya, aliitaka jumuiya hiyo kujiimarisha kwenye uwekezaji kwa kutumia vitenda uchumi walivyo navyo ili kuondokana na utegemezi ndani ya chama ikiwamo kulipa mishahara ya makatibu wake.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Dk. Edmund Mndolwa, alimwomba Katibu Mkuu Chongolo kuangalia mgawavyo wa viti maalum vya ubunge ili kuongeza nafasi kwa jumuiya hiyo.

# Siku ya Mtoto na sababu 10 kukithiri kwa ulawiti

**Na Mary Geofrey**

MABEGI ya wasichana maarufu kama 'vinainai' yametajwa kama chanzo kipya cha ukatili wa kingono kwa wanafunzi wa sekondari.

Vilevile, wanafunzi wa shule ya msingi hutumia mchezo wa 'kubambiana' kufanya vitendo vya kulawitiana chooni.

Hayo yalielezwa na Ofisa wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Kipolisi Temeke, Blandina Ndunguru, wakati akizungumza katika kilele cha Siku ya Mtoto wa Afrika kwenye Viwanja vya Mwembe Yanga mkoani Dar es Salaam jana. Alisema wasichana wamekuwa wakirubuniwa kwa kununuliwa aina hiyo ya mabegi na wanaume ambao mwisho wa siku wanawafanyia ukatili wa kingono.

"Wanafunzi wa sekondari wanapewa vinainai na kupewa lifti za bodaboda na kujikuta wakifanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono. Wanafunzi wa kiume wa shule za msingi wanalawitiana wenyewe kwa wenyewe chooni kwa mchezo wanaouita kubambiana," alisema Afande Blandina.

Alieleza zaidi kuwa matukio hayo pia yanachagizwa na wazazi wengi, hasa kinamama kuwa 'bize' na shughuli za maendeleo ikiwamo vikoba na kukosa muda wa kuangalia makuzi ya watoto wao.

Blandina alitaja sababu nyingine ni umaskini unaowafanya watoto kukosa baadhi ya mahitaji na kuingia tamaa za kutembea na wanaume ili kukidhi haja zao.

"Familia za watu wengi, wageni wanakuja wanalazwa na watoto, mama akija kushtuka, watoto wameshaharibiwa vibaya, tujifunze kuwatenga ndugu na watoto wetu kwa sababu hatujui walikotoka wamekuja na tabia zipi," alisema Blandina.

Kadhalika, alisema tatizo kubwa linaloyakabili madawati ya jinsia na watoto katika kushughulikia kesi hizo ni wazazi kutokutoa ushirikiano pindi wanapofahamu kuna tukio hilo.

Vilevile, alisema uwezekano wa kuongezeka kwa vitendo vya ulawiti kwa watoto wa kiume ni mkubwa kwa sababu wana tabia ya kulipiziana.

"Inakadiriwa kuwa ifikapo 2030 asilimia 25 ya watoto wa kiume watakuwa wamelawitiwa kwa sababu anapofanyiwa kitendo hicho, anataka naye amfanyie mwenzake," alisisitiza.

Akizungumzia takwimu za matukio hayo, alisema yanaongezeka kwa kiasi kubwa na wengi hugundulika wakiwa wameshaharibiwa vibaya.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, aliutaka uongozi wa wilaya hiyo kuhuwisha na kusimamia mabaraza ya kutoa suluhu za matukio ya ukatili kwa watoto ili kumaliza tatizo hilo.

Aliitaka jamii kujitafakari kuhusiana na malezi na mienendo ya watoto na kushamiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia na kingono.

"Utandawazi ndiyo umetufikisha hapa tulipofika, mtoto wa mwenzio akikosea huthubutu kumchapa wala kumuonya, tubadilike na kurudi kwenye misingi yetu ya awali ya kuonyana na kukemeana ili kujenga kizazi chenye maadili mema," alisema.

Mzazi Mwanaisha Ismail alisema sababu kubwa ya kukithiri kwa matukio ya ukatili wa kingono na jinsia ni kukosekana kwa hofu ya Mungu.

Alisema sababu nyingine ni migogoro ya ndoa, wazazi kutengana na mimba za utotoni, vyote vikisababisha watoto kukosa uangalizi na kuangukia mikononi mwa wahalifu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**21.03.2022**

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **14.06.2022** hadi **27.06.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili:

**KCJ943F/ZE1097, KCM104W/ZF0174**
**KBQ622Z/ZE0978, KCK293W/ZE2585**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo
**Urefu - Mita 21 Upana - Mita 4.15 Kimo - Mita 5.15**

3. Njia itakayotumika: **Holili** hadi **Moshi** kupitia **Soweto**, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

21698001

# ACT yataka CAG akague pato tozo miamala simu

**Na Moshi Lusonzo**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimemshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha zote zilizopatikana kutokana na tozo za miamala ya simu baada ya kuwapo kwa kile kilichodai mkanganyiko wa matumizi yake.

Pia kimeitaka serikali kuwachukulia hatua watu wote waliohusika na hasara ya Sh. bilioni 208 katika zao la korosho mwaka 2018.

Msemaji wa Sekta ya Fedha wa chama hicho, Emmanuel Mvula, alitoa rai hiyo jana jijini wakati akitoa tathmini ya uchambuzi wa bajeti ya serikali inayopendekezwa kwa mwaka 2022/23.

Mvula alisema jumla ya Sh. bilioni 261 zilizokusanywa kuanzia mwezi Julai 2021 hadi Machi 2022, sawa na asilimia 25.6 ya lengo ya makadirio ya trilioni 1.02, zimekuwa na mkanganyiko wa matumizi kutokana na miradi lengwa kutekelezwa na fedha za mkopo wa serikali wa kuimarisha uchumi kutokana na athari za ugonjwa wa Uviko-19 uliotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Alisema awali ACT-Wazalendo walitahadharisha kuanzishwa kwa tozo hizo kutaongeza maumivu makubwa kwa wananchi.

"Tunamshauri CAG kufanya ukaguzi maalum katika matumizi ya fedha hizi za tozo za simu kwa sababu kuna mkanganyiko mkubwa wa matumizi kutokana na ujio wa mkopo wa Uviko-19," alisema Mvula.

Alisema chama hicho pia kinaitaka serikali kufuta kabisa tozo hiyo na irudi kama ilivyokuwa kabla ya mwezi Julai mwaka 2021 ili kuwapunguzia mzigo wananchi.

Kuhusu korosho, Mvula alisema chama chake kinaitaka serikali kuwachukulia hatua wale wote waliohusika kupata hasara kutokana na kuingilia soko la zao hilo.

Alisema ili kutekeleza hatua ya serikali kununua korosho kwa wakulima, Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ilikopa Sh. bilioni 208 kwa ajili ya ununuzi baada ya watu binafsi kupigwa marufuku kununua korosho.

"Katika Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 iliyosomwa bungeni, Waziri wa Fedha ametangaza serikali kulibeba deni hilo, lakini wahusika waliosababisha hasara hiyo wapo na haijaelezwa wanafanywa nini, tunataka uwazi na uwajibikaji kufuatia uamuzi huo," alisisitiza.

Mvula alisema katika mapendekezo yao wanaitaka serikali kurudisha mapato yanayotokana na ushuru wa mauzo ya nje ya korosho ghafi ambayo wamechukua tangu mwaka 2018.

"Kabla ya mabadiliko, asilimia 65 ya mapato yatokanayo na ushuru wa mauzo ya nje yanarudi kwa wakulima kupitia mfuko wa kuendeleza zao la korosho, hivyo ni muhimu kurudisha kwa ajili ya kuongeza kiwango cha uzalishaji," alisema.

Katika uchambuzi wake, chama hicho kimegusia Deni la Taifa kikiishauri serikali kuachana na mikopo yenye masharti magumu ya kibiashara, pia kimegusa mgawanyo wa fedha za Muungano huku kikitaka waajiri na wafanyakazi wapunguziwe kilichokiita mzigo wa kodi katika mishahara.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Komredi Abdulrahman Kinana (kulia), akizungumza na Balozi wa Ubelgiji hapa nchini, Peter Van Acker, katika ofisi ndogo za makao makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: FAHADI SIRAJI WA CCM**

# Kampeni maalumu kukabili ukatili yaja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili kwa watoto na jamii, serikali imezindua kampeni maalum ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA, 2022) ili kutokomeza vitendo hivyo.

Sambamba na hilo, serikali pia imezindua mwongozo wa taifa wa uanzishaji na uendeshaji wa mabaraza ya watoto na mwongozo wa taifa wa dawati la ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alizindua kampeni hiyo jana jijini hapo kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika iliyoandaliwa na wadau mbalimbali ikiwamo Shirika la Plan International.

Alisema katika kuongeza nguvu na kasi ya kupambana kutokomeza vitendo vya ukatili kwa watoto na kwenye jamii, wizara kwa kushirikiana na wadau wake zikiwamo wizara mbalimbali za kisekta, imezindua kampeni hiyo shirikishi ya jamii.

"Dhana ya kampeni hii ni kuandikisha wanachama wengi zaidi kutoka ngazi zote na mitandao yote ya jamii wanaokerwa na uwapo wa ukatili, wenye moyo wa kujitoa bila ujira wowote kwenye kuelimisha jamii ili ifahamu juu ya uwapo wa ukatili na athari za ukatili na hatua gani wachukue kabla ya ukatili kufanyika na pale ambapo umefanyika," alisema.

Waziri huyo alisema kampeni hiyo ni huru na haina ubaguzi wowote.

"Naomba sasa kusiwe na Mtanzania anayelalamika kuhusu ukatili bila kuchukua hatua, bali sasa inuka ujiunge na SMAUJATA twende mstari wa mbele kutokomeza ukatili," alisema.

Dk. Dorothy alisema serikali pia imeanzisha mpango kazi wa taifa wa kupambana na vitendo vya ukatili dhidi watoto vinavyofanyika mtandaoni.

Kwa mujibu wa Takwimu za Jeshi la Polisi, Tanzania katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa yalikuwa 11,499 kulinganishwa na matukio 15,870 kwa mwaka 2020, kukionekana yalipungua kwa matukio 4,371, sawa na asilimia 27.5.

Alitaja mikoa iliyoongoza ilikuwa ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Mkoa wa Kipolisi Ilala (489). Alisema makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

"Kwa upande mwingine, utafiti wa serikali na UNICEF unaonyesha asilimia 60 ya matukio yanatokea nyumbani na asilimia 40 yanatokea shuleni," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Watoto wa Wizara hiyo, Sebastian Kitiku, akaulezea mwongozo wa taifa wa baraza la watoto, alisema unalenga kuwafanya watoto kutoa taarifa za ukatili dhidi yao.

# Tanzania yapewa mabilioni elimu, jamii

**Na Maulid Mmbaga**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 18.7 (Sh. bilioni 44.3) kwa ajili ya Programu ya Kunusuru Kaya Maskini awamu ya pili (PSSN) unaotekelezwa na Mpango wa Maendeleo ya Taifa (TASAF), zikisimamiwa na Ubalozi wa Sweden.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, aliipongeza EU kwa msaada huo akieleza utasaidia kupunguza upungufu wa fedha kwa ajili ya programu hiyo.

Tutuba alisema lengo la ufadhili huo ni kuwezesha PSSN kuboresha hali za kiuchumi kwa wanawake, kufadhili familia maskini kuziwezesha kupata fursa za kuongeza kipato kwa huduma za kiuchumi na za kijamii.

Alisema lengo la PSSN awamu ya pili limefikiwa kwa kiasi kikubwa hasa kwa kuwapatia kazi ya uzalishaji ili kuboresha maisha yao, kuongeza vipato na kuunda rasilimali za kijamii.

Mkuu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo wa EU, Cedric Merel, alisema: "Hatua hii inashughulikia mambo kadhaa ya msingi yanayozuia wanawake na wasichana kutumia haki zao na kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania."

Wakati huo Serikali ya Italy imeipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Euro 19,790,400 (Sh. bilioni 49.1) pamoja na msaada wa Euro 200,000 (Sh. milioni 496.5) kwa ajili ya programu ya kuendeleza taasisi za ufundi za elimu ya juu nchini.

Akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini mkataba huo jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema mradi huo unalenga kuanzishwa kwa vituo vya ujasiriamali, ubunifu na kukuza teknolojia katika taasisi nne za ufundi za elimu ya juu.

Tutuba alizitaja taasisi zitakazonufaika na fedha hizo ni Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam – (DIT), Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar (KIST) na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).

Alisema fedha hizo zitakuza ari ya ujasiriamali ambayo itawezesha kukua kwa teknolojia nchini na hivyo kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana kwa kuwawezesha wahitimu wa vyuo hivyo kuwa na ujuzi wa biashara.

Balozi wa Italy nchini, Marco Lombardi, alisema Italy itaendelea kuisaidia Tanzania katika sekta mbalimbali na kwamba mkopo huo nafuu utakwenda kusaidia sekta ya elimu nchini.

# Watakaohama Ngorongoro wahakikishiwa huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jimmy Yonazi, amewahakikishia wakazi wa Kijiji cha Msomera na wageni watakaohamia kutokea Ngorongoro uhakika wa kupata huduma bora za mawasiliano wawapo kijijini hapo.

Akizungumza katika ziara ya kukagua upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kijiji cha Msomera jana, Dk. Yonazi, alisema serikali inatambua umuhinu wa mawasiliano katika kukuza uchumi na wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake na kuwa wamejipanga kuhakikisha mawasiliano hayayumbi.

Dk. Yonazi aliagiza Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), kuhakikisha kuwa inawaelekeza watoa huduma wote wa mawasiliano kwenda kuwekeza na kutoa huduma za mawasiliano kijijini hapo ili watumiaji wapate wigo mpana zaidi wa kuchagua.

Akipokea maagizo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, alisema TCRA itatekeleza agizo hilo mara moja na kuongeza kuwa katika kuitikia wito wa kuboresha mawasiliano, itafadhili maabara ya TEHAMA yenye kompyuta 23 na huduma za mtandao wa intaneti katika Shule ya Sekondari ya Msomera.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote USCAF, Justina Mashiba, alisema mfuko wao utafadhili maabara ya TEHAMA katika shule ya msingi hiyo ikiwa ni hatua ya kuwajengea msingi wa TEHAMA kuanzia wakiwa wadogo.

Akizungumzia maendeleo ya matayarisho ya Kijiji cha Msomera kupokea wageni kutoka Ngorongoro, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, alisema Kijiji cha Msomera kipo tayari kupokea wageni na huduma zote za msingi ikiwamo makazi, maji, umeme, shule, majosho na maji kwa ajili ya mifugo vipo tayari.

# W'biashara wampa kongole Samia kusitisha ukaguzi kodi zaidi miaka 5

**Na Mwandishi Wetu**

UAMUZI wa RAIS Samia Suluhu Hassan, kusitisha ukaguzi na utozaji wa kodi za nyuma zaidi ya miaka mitano iliyopita umeungwa mkono na wafanyabiashara na jumuiya ya wafanyabiashara, wenye viwanda na wakulima Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, Ofisa Uhusiano wa Jumuiya ya Wafanyabiashara visiwani humo, Mafuda Faki, alisema uamuzi huo utasaidia kuondoa usumbufu waliokuwa wakiupata.

"Kumkagua mtu kodi na kumtoza za zaidi ya miaka mitano nyuma, wengine walikuwa wanashindwa kumudu na kufikia kufunga biashara zao," alisema Mafuda.

Alisema ukaguzi wa mwaka mmoja wa kodi za nyuma kama utafanyika alivyoagiza Rais Samia utasaidia kuondoa usumbufu na serikali kuwa na takwimu sahihi za ukusanyaji wa kodi na muhimu mamlaka za kodi ziwe na watendaji wa kutosha, vifaa na wataalamu wa kusimamia vifaa vya teknolojia na ukusanyaji.

"Nakubaliana na Rais Samia kutofanya ukaguzi wa miaka mitano ya nyuma ni uzembe kwa wakusanya kodi, lakini ni mzigo mkubwa kwa walipa kodi kwa vile wengi viwango wanavyopelekewa wanashindwa kuvimudu na kuteteresha biashara zao jambo ambalo sio zuri kwa maendeleo ya sekta ya biashara," alisema Mafuda.

Akizungumza na waandishi wa habari, mchambuzi wa masuala ya uchumi, Abdul Mshangama, alisema kwa kuwa masuala ya fedha ni mambo ya Muungano Zanzibar pia inapaswa kutekeleza agizo la Rais Samia.

"Masuala ya fedha ni mambo ya Muungano na sera ya fedha inasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania, agizo la Rais linapaswa kutekelezwa na Zanzibar kwa sababu imekuwa kero kwa wafanyabiashara," alisema Mshangama.

Kadhalika, alisema mpaka sasa kuna wafanyabiashara wanakaguliwa ripoti za malipo ya kodi za miaka mitatu hadi mitano ya nyuma na kusababisha usumbufu mkubwa na wengine kushindwa kumudu nyongeza ya kodi wanazotakiwa kulipa.

Pia, alimpongeza Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi kwa juhudi anazoendelea kuchukua za kuondoa kodi mbalimbali katika maeneo ya huduma za jamii pamoja na tozo kwa wajasiriamali ili kuwainua kibiashara.

"Kama agizo la Rais Samia litatekelezwa kwa vitendo na mamlaka za ukusanyaji wa kodi maendeleo katika sekta ya biashara na utalii yataweza kupatikana kwa sababu hata wawekezaji imekuwa kero kwao," alisema Mshangama.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wafanyabiashara Zanzibar, akiwamo Ahmed Suleiman Nassor na Muhammed Abdulrahman Bajuber, walisema tatizo la kutozwa kodi la zaidi ya mwaka mmoja nyuma limekuwa sugu na kurudisha nyuma maendeleo ya sekta ya biashara.

"Kuna watu wanapelekewa madai ya nyuma makubwa na wanaposhindwa kumudu kulipa ndipo unaposikia mtu kafunga biashara yake," alisema Bajuber.

Hata hivyo, alisema ili agizo la Rais Samia liweze kutekelezwa, lazima kuwapo na uwiano wa watendaji, vifaa ili ukaguzi wa kodi ufanyike kwa wakati kwa sababu hivi sasa wafanyabiashara ni wengi kuliko watendaji wa ukaguzi wa kodi katika mamlaka ya dhamana.

"Rais Samia anapaswa kupongezwa kwa sababu amekuja na jibu mwafaka la kulinda maendeleo ya sekta ya biashara," alisema mfanyabiashara maarufu Ahmed Suleiman Nassor.

Kwa upande wake, Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar, Juma Bakari Hassan, alisema agizo la Rais wamelipokea na linafanyiwa kazi kabla ya utekelezaji kuanza kutumika mwaka huu.

Alisema Zanzibar ina wafanyabiashara karibu 20,000 waliosajiliwa kodi huku wafanyakazi wa Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) Zanzibar wakiwa 150.

Hata hivyo alisema mifumo ya kisasa ya kielektroniki ya kulipa kodi imerahisisha ukusanyaji pamoja na kuziba mianya ya ukwepaji.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum alisema, watakaa na kujadili kuhusu agizo la Rais Samia kabla ya kutoa msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.



Wakulima wa mpunga Matha Mgomba (kushoto) na Penina Mtulia, wakivuna zao hilo, kwenye shamba lao wilayani Kibaha mkoani Pwani mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wabunge wataka magari ya serikali kutumia gesi

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Bajeti, imependekeza magari ya serikali yawe na mfumo wa kutumia gesi asilia kama ilivyo kwa malori ya kampuni ya Dangote.

Aidha, imebainisha changamoto za ubia kati ya serikali na sekta binafsi katika kutekeleza miradi, huku ikitaka kuwapo sera na sheria ya tathmini na ufuatiaji.

Hayo yamo kwenye taarifa ya kamati hiyo kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2021, tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya serikali mwaka 2021/22 na mpango wa maendeleo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/23.

Akiwasilisha taarifa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Daniel Sillo, alisema hatua hii sio kwamba itapunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje, vilevile itapunguza nakisi ya urari wa jumla wa malipo na biashara.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia iitwayo Reinvigorating Growth in Resource-Rich Sub-Saharan Africa ya mwaka 2018, Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 Afrika zenye rasilimali nyingi.

"Uwapo wa rasilimali sio kigezo pekee cha kuwa na maendeleo. Ili maendeleo yapatikane ni lazima rasilimali hizo zitumike kwa ajili ya shughuli mbalimbali," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuendelea kuwa na rasilimali ambazo hazitumiki, hakulihakikishii taifa maendeleo. "Ni muhimu sana kama taifa kufanya mabadiliko katika matumizi ya rasilimali tulizonazo. Nchi nyingi hivi sasa zinahama katika matumizi ya nishati zinazozalisha hewa ukaa na kwenda kwa nishati jadidifu," alisema.

"Kuna baadhi ya rasilimali tusipozitumia hivi sasa huko mbeleni zinaweza zisiwe na thamani, mfano makaa ya mawe. Ni vyema sasa serikali ihakikishe rasilimali hizi zinavunwa kwa uangalifu na kwa maslahi mapana ya taifa," alisema.

**CHANGAMOTO PPP**

Sillo alisema kamati ilifanya tathmini ya ubia baina ya sekta ya umma na binafsi na kubaini changamoto za utekelezaji ambazo ni kiwango cha chini cha mtaji unaotambulika kisheria kwa ajili ya miradi ya PPP ni Dola za Marekani milioni 20 sawa na Sh. bilioni 40.

Nyingine ni mwamko mdogo wa wizara, idara na taasisi za umma kutekeleza miradi kwa njia ya ubia na mazingira mabovu ya uwekezaji ambayo hayavutii uwekezaji kwenye miradi ya aina hiyo.

Aidha, alisema nyingine ni ugumu uliopo kisheria wa kutekeleza miradi kwa njia hii hasa ile miradi inayoibuliwa na sekta binafsi na inayopendekezwa ifanyike kwa ubia na serikali.

"Kamati inaishauri serikali kuhakikisha inatanzua vikwazo vilivyobainishwa, ili lengo la utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia lifanikiwe," alisema.

Alisema pia, kamati katika uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo imebaini baadhi ya wizara, idara na taasisi za serikali hazifanyi kazi kwa kushirikiana.

"Mfano mradi wa umeme vijijini unatekelezwa na wakala wa umeme vijijini, lakini jambo la kushangaza ni pale ambapo tathmini ya maeneo yanayohitaji kuunganishiwa umeme inafanyika na taasisi za umma kama vile shule, hospitali na zahanati hazijumuishwi," alisema na kuongeza:

"Eneo jingine ni pale ambapo halmashauri inapanga kujenga hospitali ya wilaya lakini Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA), TANESCO na Mamlaka ya Maji ya eneo husika kutokuwa na mpango wala bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kupelekea huduma hizo muhimu katika hospitali."

Alisema kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwenye miradi ya umma ni vyema taasisi zote zikashirikiana, ili kupunguza gharama za mradi na kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.

**SERA YA UFUATILIAJI**

Mwenyekiti huyo alisema ni muhimu serikali ikaandaa sera ya taifa ya ufuatiliaji na tathmini na baadaye kutunga sheria yake.

"Ufanyaji wa ufuatiliaji na tathmini ni zoezi la kitaalamu ambalo lina malengo makuu matatu moja ni kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa, mbili ni kuhakikisha kunakuwa na thamani ya fedha na tatu ni kurekebisha mapungufu wakati wa utekelezaji wa mradi au shughuli yoyote," alifafanua.

Alisema kwa miaka mitatu mfululizo kamati imekuwa ikishauri serikali kuandaa sera hiyo, ili baadaye itungiwe sheria.

"Kutokufanya hivyo kumeacha ombwe katika ufuatiliaji na tathmini na badala yake serikali imekuwa ikiziba ombwe hilo kwa kuandaa miongozo kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini," alisema na kuongeza:

"Sababu za msingi za kuomba uwapo wa sera na sheria ni kuhakikisha majukumu ya kila mmoja yanabainishwa na adhabu zake. Hatua hii itaondoa changamoto zilizoko katika utekelezaji wa miradi," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Siku ya Mtoto wa Afrika tumlinde dhidi ya ukatili

**KILA** mwaka Juni 16, mataifa, jumuiya mbalimbali za kimataifa pamoja na wadau hukusanyika pamoja kwa ajili ya kujadili fursa na changamoto zinazowakumba watoto katika bara la Afrika.

Hapa nchini shughuli hiyo inafanyika katika sehemu mbalimbali mikoani kwa wadau kutoa elimu iwe kupitia warsha, semina na maonesho.

Watoto wanakumbana na changamoto mbalimbali katika jamii ikiwamo kufanyiwa vitendo vya ukatili, iwe majumbani, shuleni na hata katika maeneo wanayocheza.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na taasisi mbalimbali za kutetea haki za watoto, wengi hukumbana na changamoto hizo kutoka kwa ndugu zao wa karibu na baadhi ya wazazi pia uhusishwa na vitendo hivyo.

Siku hii ilianza kuadhimishwa tangu mwaka 1991 ilipoteuliwa na Umoja wa Afrika kuenzi michango ya watoto walioshiriki katika maandamano mji wa Soweto, Afrika Kusini mwaka 1976 kupinga mauaji ya watoto wenzao na pia kujengea jamii uelewa juu ya umuhimu wa elimu bora kwa watoto.

Tanzania kama nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika imekuwa ikiadhimisha siku hii tangu mwaka 1991. Lengo la kuadhimisha siku hii ni kukumbuka mauaji ya kinyama waliyofanyiwa watoto wa kitongoji cha Soweto.

Maadhimisho haya ni fursa ya kutathmini utekelezaji wa Sera za Taifa zinazohusu maendeleo ya watoto kwa kuwapatia huduma stahiki ikiwa ni pamoja na afya, elimu, ulinzi na malezi bora ili kuwarithisha stadi mbalimbali na tunu za kitaifa kwa manufaa yao, familia na taifa kwa ujumla.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni "Maendeleo Endelevu 2030: Imarisha Ulinzi na Fursa Sawa kwa Watoto" Kaulimbiu hii inawataka wazazi, walezi, serikali na wadau wengine kuzingatia wajibu katika kuimarisha mifumo ya ulinzi na maendeleo ya mtoto ili aweze kudhibiti changamoto ya ongezeko la vitendo vya ukatili nchini pamoja na kutoa haki sawa kwa watoto wote bila ubaguzi wa aina yoyote.

Maadhimisho haya yawe chachu kwa jamii kuwalinda watoto bila kujali kama umemzaa wewe. Kuna msemo unaosema mtoto wa mwenzako ni wa kwako hivyo, kila unapomuona mtoto akifanyiwa unyama au udhalilishaji na ukatili wa aina yoyote, wajibu wako ni kumnasua katika hali hiyo kwa kuripoti kwenye vyombo vinavyotakiwa ili hatua ichukuliwe mara moja.

Vitendo vya ukatili wa watoto vinaendelea kushamiri maeneo mbalimbali nchini kutokana na jamii kutolibeba jukumu la malezi kwa watoto hao. Mtoto akionekana anafanyiwa ukitili baadhi ya jamii huliacha bila kuchukua hatua na kusababisha waendelee kupata mateso na kukosa haki zao za msingi ikiwamo uhuru wa kuishi.

Watoto wengine wanakosa haki ya kupata elimu kwa sababu ya kutumikishwa kazi za nyumbani au kufanyiwa vitendo vya kinyama vya kutumikishwa kingono.

Kama jamii itajitwisha jukumu la maelezi bila kujali kwamba mtoto huyo sio wa kwako, tatizo la ukatili litapungua.

Hii itasaidia hata mtu anayetaka kumfanyia ukatili mtoto kuogopa kwa sababu atakuwa anajua kuna watu wanamwangalia. Kwa pamoja tukishikamana tatizo hili la ukatili wa watoto litatokomezwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wananchi tuwe makini sana na pesa za mitandaoni

Na Adam Fungamwango

**NI** majonzi na vilio kwa baadhi ya Watanzania waliojiunga kwenye programu maarufu ya mtandaoni iitwayo 'Idea Debater' kwa lengo la kuvuna fedha, badala yake wakajikuta wakitapeliwa fedha hizo kwa kuwa baadaye programu ilifungwa.

Mwezi Machi mwaka huu, programu hiyo iliwaunganisha mamia kwenye makundi ya 'Whats App' na kwa bahati nzuri au mbaya ikapata umaarufu wa ghafla baada ya Watanzania wengi kujiunga nayo kwa kufuata maelekezo na kujaza maelekezo na taarifa muhimu zinazohitajika.

Walioingia kwenye mchezo huo wanasema ili upate faida ya kamisheni ya kila siku ya asilimia tano hadi nane kwa kukamilisha kazi 20 za kuweka oda kila siku, mtu mmoja alitakiwa kuweka salio kwenye akaunti na inapofika saa 8:00 usiku oda mpya zilikuwa zimewekwa.

Kuna baadhi ya watu wa kwanza ambao walivuna fedha, lakini walikuwa wakiongeza kiwango kila siku zinavyozidi kusonga mbele mpaka siku ambayo jamaa waliamua kufunga programu.

Huu ni moja ya mlolongo wa utapeli ambao Watanzania wameendelea kuathirika nao, ukiwamo wa miaka kadhaa uliopita DECI. Tatizo hasa ni nini?

Kwanza kabisa inaonekana kuwa baadhi ya watu hawana kazi, hivyo wanacheza michezo hii na mingine ili kujipatia kipato.

Cha ajabu ni kwamba hata mchezo huu umechezwa na watu wengi ambao ni wafanyakazi na wafanyabiashara. Hii inaonyesha kuwa baadhi ya Watanzania wanapenda kupata pesa nyingi kwa urahisi na bila kuzifanyia kazi.

Mara nyingi matapeli hutumia sana mwanya huu. Na yoyote yule ambaye anapenda kupata, au kuingiza pesa nyingi bila utaratibu unaoeleweka, ni rahisi sana kudanganywa na kutapeliwa.

Yupo mama mmoja aliuza nyumba, hao hao waliouziwa baadhi yao walimzunguka na kumwambia kuna mganga ambaye anaweza kuziongeza pesa hizo mara mbili zaidi ya hizo zilizoko.

Wakamshawishi mama huyo, hivyo pesa zile akazipeleka zote kwa mganga ili zizae na kama zipo Sh. milioni 200, basi ziwe Sh. milioni 400. Kilichotokea ni kwamba hata zile alizochukuliwa na nyumba ikaenda kwa sababu tayari alikuwa ameiuza.

Ukweli ni kwamba zile pesa zilirudi kwa wale wale walioinunua.

Kwa maana hiyo, nyumba ile wakawa wameichukua bure. Mama akabaki na kilio pamoja na kusaga meno. Tatizo lake lilikuwa ni dogo tu, kutaka pesa kwa njia ya mkato. Kutaka kupata pesa nyingi kwa muda mfupi na kwa njia ya urahisi bila kutoka jasho.

Watu wengi wametapeliwa kwa njia hii. Ukweli ni kwamba, hata kwenye vitabu vitakatifu imeandikwa binadamu atakula kwa jasho. Ina maana duniani. hakuna kitu rahisi.

Chochote utakachokiona kina urahisi hebu jaribu kufikirisha akili, kufanya uchunguzi mdogo na kukifuatilia kama kina ukweli, badala ya kuingia moja kwa moja kutokana na maneno matamu na ushawishi.

Watu wanatapeliwa kwenye mitandao ya kijamii, simu za mkononi, kwa waganga wa kienyeji na hata laivu tu, lakini bado wengine wamekuwa hawajifunzi licha ya vyombo vya habari kutangaza na kutahadharisha mara kwa mara.

Katika dunia hii, waliotajirika au kupata pesa nyingi kwa njia kama hizo inawezakana ikawa ni asilimia mbili tu, lakini fuatilia matajiri wote, au watu wenye uwezo wa kifedha, ikiwamo wafanyabiashara ni kwamba wamezipata kwa jasho.

Wamewekeza kwenye biashara mbalimbali na wakati mwingine kupata hata hasara, lakini mwisho wa siku wamefanikiwa.

Hata mitaji yao inakuwa ni mikubwa kuliko hata faida wanazopata. Lakini sisi tunataka faida kubwa kwa muda mfupi bila mtaji.

Hata Msemaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja, alionyesha kusikitishwa kuona watu wanaendelea kutapeliwa, wakati serikali ilishapiga marufuku masuala ya upatu na mengine yanayofanana na hayo, bado yanaendelea kutokea.

Akawataka wanaotaka kuwekeza kupeleka fedha na mitaji yao kwenye taasisi zinazotambuliwa kisheria, yakiwamo masoko ya hisa.

Nimalize kusema, Watanzania sasa ni lazima waamke, wawe makini, hakuna pesa rahisi kiasi hicho kwenye dunia hii na dunia haijawahi kuwa rahisi kihivyo, chochote kile ni lazima upambane, na kitakachoonekana kuwa rahisi ni lazima uwe na wasiwasi nacho.

## RC, benki wafunda wafanyabiashara

**Na John Badi**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, ameungana na maofisa waandamizi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kuwafunda wafanyabiashara wakubwa na wadogo wa jijini Mwanza jinsi ya kukuza biashara zao kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na NBC kwa ajili ya wateja wadogo na wakubwa wa jijini humo, Gabriel aliwashauri wafanyabiashara hao kuhakikisha wanatumia vyema huduma za kifedha zinazotolewa na NBC kukuza mitaji yao ili kujiongezea faida zaidi.

"Kikubwa ni kuhakikisha tu kwamba kila unachokifikiria kukifanya kuhusu biashara, ukifikirie kwa ukubwa wake. Kama ni biashara ya duka, basi hakikisha unafungua duka kubwa lenye huduma nzuri na za kisasa ili kuvutia na kuhudumia wateja wengi iwezekanavyo ili kukuza mtaji wako lakini pia uweze kuvutia taasisi za kifedha zishawishike kuendelea kukuunga mkono," alisema

Hafla hiyo ililenga kujadili fursa za biashara na kutambulisha huduma mpya za benki hiyo kupitia klabu yake ya biashara inayofahamika kama NBC Business Club.

Mkuu wa Kitengo cha Wajasiriamali wa NBC, Mussa Mwinyidaho, alisema benki hiyo imedhamiria kuboresha huduma zaidi ili wateja wake waendelee kufurahia huduma zilizorahisishwa zaidi ili kuendana na matakwa ya kukuza biashara zao.

"Ni kutokana na ubunifu wa huduma na fursa mpya kila mara ndio sababu tumekuwa na huu utaratibu wa kukutana na ninyi wateja wetu ili kuwasilisha kwenu huduma hizi mpya.

"Kupitia huduma yetu ya NBC Business ClUB, tunaweza kutangaza huduma mpya kwa ajili ya wajasiriamali ikiwamo huduma ya 'Commercial Property Financing' inayowawezesha wajasiriamali wenye majengo ya biashara kupata mikopo yenye marejesho nafuu sambamba na huduma ya 'Commercial Asset Financing' inayowawezesha wajasiriamali hao kukopa mitambo kwa ajili ya biashara na shughuli za ukandarasi.

"Pia, kupitia tukio hili la leo wateja wetu jijini Mwanza watapata fursa ya kufahamu huduma zetu za mikopo bila dhamana ikiwpo huduma ya 'Distributor financing' inayowawezesha wajasiriamali kupata mikopo ya kusambaza bidhaa zao bila dhamana pamoja na huduma ya 'Purchasing Order Financing' inayowawezesha wajasiriamali kupata mikopo kwa kutumia hati ya ununuzi, yaani LPO," alisema.

# Watoto na wanawake 280 wafanyiwa ukatili

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JUMLA ya watoto na wanawake 280 katika kata ya Bugarama Halmashauri ya Msalala, wamefanyiwa vitendo vya kikatili kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni, mwaka huu hali inayosababisha walio na umri wa kwenda shule kushindwa kuendelea na masomo.

Hayo yalibainishwa na Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Bugarama, Dk. Silasi Kayanda, wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa kituo cha pamoja cha kuhudumia waathirika wa ukatili wa kijinsia kinachojengwa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa Tanzania ambayo ni UNFPA, UNWomen kwa ufadhili wa KOICA.

Alisema, vitendo vya kikatili kwa watoto na wanawake vimeshamiri katika kata hiyo na mwaka jana matukio 705 yaliripotiwa na kupatiwa huduma, takwimu hizo ni za wanaojitokeza kupata huduma baada ya kufanyiwa ukatili.

Kayanda alisema, kutoka kituo hicho mpaka polisi ni umbali wa kilometa tano huku ofisi za Ustawi wa Jamii zikiwa umbali wa kilometa 70 hali ambayo wanaofanyiwa vitendo vya kikatili kushindwa kufika vituoni kwa wakati na wengine kulazimika kukata tamaa kwa kuhofiwa kutengwa na familia zao. Ofisa Ustawi wa Jamii, Halmashauri ya Msalala, Richard Ng'ondya, alisema licha ya kuendelea kutoa elimu ya kupinga vitendo vya kikatili, vimezidi kuongezeka kila siku na kwa mwezi yamekuwa yakiripotiwa matukio 10 hadi 15 na kwamba kitakapokamilika kituo hicho na kuanza kutoa huduma kitasaidia kupunguza wimbi la matukio hayo.

Alisema, vitendo vya ubakaji, ulawiti na vipigo kwa kinamama vimeshika kasi kata zote za Halmashauri ya Msalala na wengi wanashindwa kutoa taarifa kutokana na umbali wa kituo cha polisi na ofisa ya ustawi wa jinsia.

Awali, akisoma taarifa ya ujenzi wa kituo hicho, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali KIWOHEDE, Justa Mwaituka, alisema kituo hicho kitakapokamilika kitagharimu Sh. milioni 95 na kinatarajia kukamilika Juni 30 na kuanza kutoa huduma.

Kwa upande wa Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Mark Bryan Schreiner, alisema wanashirikiana na serikali kupambana na vitendo vya kikatili ndani ya jamii nchini kwa kutoa elimu ya ujasiriamali, kilimo na afya kwa sababu vitendo hivyo vinasababishwa na umaskini ndani ya familia.

Alisema, ili kuendelea kupambana na vitendo hivyo, watajenga vituo vingine viwili katika Wilaya ya Ikungi mkoani Singida na Shinyanga lengo likiwa ni kusogeza huduma karibu na wananchi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, alisema anatamani vituo hivyo vingejengwa kila kata mkoani hapo kusaidia kupambana na vitendo vya ukatili ndani ya jamii.

Alisema, wanafanyiwa ukatili na kushindwa kutoa taarifa kwa hatua zaidi za kisheria kwa sababu ya umbali mrefu wa vituo vya polisi, ofisi za ustawi wa jamii na madawati ya jinsia.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Prof. Evaristo Liwa (kulia), akisaini waraka wa makubaliano na Mkuu wa Kitivo cha Usanifu Majenzi wa Chuo cha Leoven cha nchini Ubelgiji, Prof. Yves Schoonjans, mkoani Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya vyuo hivyo kushirikiana kwenye nyanja mbalimbali. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kituo kuhamasisha sensa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wanawake na Makundi Maalumu, Mwajuma Magwiza, amekitaka Kituo cha Taarifa na Maarifa, Kata ya Shilela, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, kuwahamasisha wananchi kushiriki sensa Agosti 23, mwaka huu.

Magwiza alitoa rai hiyo jana wakati wa ukaguzi wa miradi inayotekelezwa kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia Halmashauri ya Msalala, inayotokelezwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini, UNFPA na UN-Women kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la nchini Korea (KOICA).

Miradi hiyo ni pamoja na kituo cha kuhudumia waathirika wa ukatili wa kijinsia, klabu ya wasichana ya kupinga ukatili wa kijinsia, kituo cha taarifa na maarifa, choo katika soko la Segese na kikundi kinachojihusisha na kilimo cha mboga na matunda.

Alisema, nguvu inayotumika kupambana na vitendo vya kikatili ndani ya jamii itumike pia kuwahamasisha wananchi kushiriki sensa ya watu na makazi kwa kuwapatia elimu ikiwa ni pamoja kuacha tabia ya kuwaficha watoto wenye ulemavu.

Aidha, Magwiza alisema wakati kituo hicho kinafanya kazi hiyo ni vyema wakashirikiana na maofisa maendeleo ya jamii waliopo kila kata kuhakikisha ujumbe unawafikia wananchi wote na lengo la serikali ni kuona wananchi wote wanashiriki bila ubaguzi kwa ajili ya maendeleo yao.

"Tusiwafiche watoto wetu wenye ulemavu wakati wa zoezi la sensa ya watu na makazi kwani nao wana haki ya kuhesabiwa kama walivyo wengine na kufanya hivyo ni kwenda kinyume na haki za binadamu na ukibainika unaweza hata kushtakiwa," alisema Magwiza.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kata ya Shilela, Mwanaidi Mzee alisema, kituo cha taarifa na maarifa kata kina jumla ya wajumbe 120, wa kiume wakiwa 20 na wote na watatawanya mitaa yote kuhakikisha wanatoa elimu ya mapambano ya ukatili na kushiriki sensa ya watu na makazi.

Vile vile, alisema, kupitia vikao vya kukumbusha wajibu wa kazi vinavyofanyika kila wiki, suala la sensa wameliweka kama ajenda ya kudumu na wamekuwa wakiwashirikisha wenyeviti wa vijiji, vitongoji ngazi ya jamii na wana uhakika wananchi wote watashiriki kwa wingi.

Naye mjumbe wa kituo hicho, Agnes John alisema, awali wakati akitoa elimu ya mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike hususani mimba za utotoni walikuwa wanakutana na vipingamizi kutoka kwa wazazi kwa sababu ya imani ya mila potofu ya kuwaozesha wakiwa na umri mdogo.

Mwingine, Mabula Emmanuel alisema, wamekuwa wakitenga muda wa kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia na sensa ya watu na makazi na wananchi wanaonyesha kuitikia na wamekuwa wakiwaahidi kutoa taarifa endapo itabainika familia kusafirisha watoto wenye ulemavu.

# UBA yatoa msaada wa vitabu sekondari

**Na John Badi**

BENKI ya UBA kupitia mpango wake wa Read Africa Initiative, imeungana na ulimwengu kusherehekea Siku ya Mtoto wa Afrika kwa kuchangia vitabu vya fasihi katika Shule ya Sekondari Kurasini mkoani Dar es Salaam.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wakubwa wa Benki hiyo, Dora Kyungu, alitumia fursa hiyo jana kuelezea mpango huo na mchango wake katika kuwahamasisha wanafunzi barani Afrika kuboresha msamiati wao na uwezo wa kuwasiliana kupitia usomaji.

"UBA ni benki inayofanya kazi katika maeneo mbalimbali duniani ikiwamo Uingereza, Marekani na Ufaransa na pia inapatikana katika nchi 20 barani Afrika.

"Benki hii inatambua jinsi tamaduni za kusoma zilivyo muhimu kwa ajili ya maisha ya baadaye ya watoto waliopo barani Afrika na duniani kote.

"Watoto wote wanahimizwa kujenga tabia ya kusoma vitabu ili waweze kutajirisha hifadhi ya msamiati na kukuza uwezo wao wa kujifunza," alisema Dora. Akizungumza baada ya kupokea vitabu hivyo, Mkuu wa Shule hiyo, Amry Jaribu Fundi, aliishukuru benki hiyo kwa mchango wake kwenye elimu bora nchini na kuwahimiza wanafunzi watumie fursa hiyo ili kukuza uelewa wao na kuendeleza hulka ya usomaji wa vitabu.

Dada Mkuu wa Shule hiyo, Sonia Madaha, alitoa shukrani kwa niaba ya wanafunzi wenzake na kuahidi kuendelea kuongoza kwa mfano kwa kusoma zaidi.

Juni 16 kila mwaka ni siku maalum iliyotengwa na Umoja wa Mataifa kama Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Afrika ili kusherehekea watoto barani Afrika pamoja na kutambua ujasiri wa wanafunzi walioandamana kwa ajili ya suala la elimu bora jijini Soweto, Afrika Kusini.

# DC apiga marufuku watoto kufanyishwa biashara

**Na Happy Mollel,** BARIADI

MKUU wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Lupakisyo Kapange, amepiga marufuku watoto (wanafunzi) kufanya biashara katika maeneo ya migodi, minada na sokoni.

Aidha, amewataka maofisa wa polisi kuchunguza na kusimamia suala hilo ili kubaini wazazi na ndugu wanaowatumikisha kibiashara wanafunzi hao kwa manufaa yao wenyewe.

Kapange alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika katika viwanja vya halmashauri mjini humo.

Alisema kuna baadhi ya ndugu na wazazi wenye tabia ya kuwatumikisha kibiashara watoto hao kwenye maeneo mbalimbali ya kibiashara hasa nyakati za jioni na kuwataka kuacha mara moja.

Pia, alisema wanaanza kufanya msako rasmi na kuwakamata wazazi wenye tabia hiyo.

"Ninasikitika sana kusema katika Wilaya ya Bariadi kuna tatizo la wazazi kuwafanyisha kazi za kibiashara watoto wao hasa nyakati za jioni wanaporudi nyumbani...niwaombe waache mara moja kwani tunaanza kufanya msako maalum na endapo tutabaini, tutakamata wazazi wa namna hiyo ili wawe mfano kwa wengine...na kwa kufanya hivyo watoto watapata fursa ya kutimiza malengo yao waliyojiwekea," alisema Kapange.

Aliwaonya walimu wanaoshiriki kuvuruga na kuharibu kesi za ubakaji shuleni kwa kuwa kufanya hivyo ni kuingilia uamuzi wa mhimili mwingine.

Aliwataka walimu kumpatia orodha ya wanafunzi wa shule ya msingi ambao walitakiwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu na mpaka sasa hawajawasili ili waweze kufuatiliwa waliko.

Akisoma taarifa fupi katika maadhimisho hayo, ofisa maendeleo ya jamii, Janeth Jackson, alisema wanashirikiana na jeshi la polisi kuhakikisha ulinzi na haki za watoto zinatekelezwa vyema.

Alisema kwa mwaka 2021/2022 idara yake ilipokea mashauri 90 ya watoto na kati ya hayo 68 yalipata suluhu, 17 yalipatiwa rufaa na matano yako katika ngazi ya mahakama.

Nao baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi Sima na Bariadi, walisema wanaomba ulinzi uimarishwe dhidi yao ili waweze kutimiza ndoto zao.

"Sisi wanafunzi tunaomba ulinzi dhidi yetu...na vitendo vya kikatili vitokomezwe kwani matukio ya ukatili, ubakaji na unyanyasaji yamekuwa mengi," alisema mmoja wa wanafunzi hao Zulfa Hamis.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wakubwa wa Benki ya UBA, Dora Kyungu (kushoto), akikabidhi msaada wa vitabu zaidi ya 300 kwa Dada Mkuu wa Shule ya Sekondari Kurasini, Sonia Madaha, kwa ajili ya shule hiyo, mkoani Dar es Salaam jana, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Afrika. Wapili kushoto ni Ofisa Masoko na Mawasiliano wa UBA, Valdy Khahima na (wapili kulia) ni Kaka Mkuu wa shule hiyo, Fredrick Halilu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuwasaka na kuwakamata waliowaua wazee popote

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali itahakikisha inawasaka na kuwakamata popote walipo hata kama wamekimbilia nje ya nchi waliohusika na mauaji ya wazee watatu wilayani Iramba mkoani Singida.

Aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya kupinga ukatili kwa wazee yaliyofanyika kitaifa katika Kijiji cha Kisharita, Wilaya ya Iramba mkoani Singida ambako kulifanyika mauaji ya wazee watatu wenye umri kati ya miaka 80 hadi 84.

Machi 26 mwaka huu, wazee watatu wa Kijiji cha Kisharita Wilaya ya Iramba; Agnes Msengi (84), Widina Said (80) na Winfrida Ndigina (80) waliuawa kikatili na watu wasiojulikana kutokana na imani za kishirikina.

Hadi sasa waliohusika katika mauaji hayo hawajakamatwa, hatua ambayo ilimfanya Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri wa Wazee Manispaa ya Singida, Juma Mudida, kuhoji kwa waziri ni kwanini watuhumiwa hawajakamatwa.

"Dhahabu iko chini ya ardhi, kilomita nyingi lakini inatafutwa kwa kuchimba na inapatikana, inakuwaje inashindikana hadi sasa kupatikana kwa watuhumiwa waliosababisha vifo vya wazee hawa?" Mudida alihoji.

Akijibu hoja hiyo, Dk. Gwajima alisema wote waliohusika na mauaji hayo watasakwa kwa kutumia askari wa kimataifa ikibidi kama wahusika watakuwa wamekimbilia nje ya nchi.

Alisema serikali imeendelea na juhudi za kupambana na ukatili kwa wazee kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwamo Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawane na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18-2021/22 na Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Mauaji Dhidi ya Wazee 2018/19-2022/23.

Alisema kwa takwimu zilizopo katika Jeshi la Polisi, mwaka 2021 hakuna mzee aliyepoteza maisha kwa mauaji lakini mwanzoni mwa mwaka 2022 mwanzoni, nchi iliingia katika dosari kubwa kutokana na mauaji ya wazee yaliyotokea katika mikoa mbalimbali kutokana na sababu mbalimbali zikiwAmo za kiuchumi na imani za kishirikina.

Dk. Gwajima alitumia fursa hiyo kuziagiza halmashauri zote nchini kuitumia Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA) ili isaidie kutokomeza vitendo vya ukatili kwenye halmashauri.

Kuhusu matibabu kwa wazee, alisema serikali imewapatia vitambulisho vya bima za afya vya msamaha wa matibabu wazee 937,266 ambao ni kati ya 1,547,038 waliotambuliwa katika mikoa 26 nchini.

Alisema serikali imewapatia vitambulisho hivyo wazee ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kimaendeleo na za kijamii kutokana na kutambua na kuthamini mchango wa wazee na kuhakikisha ulinzi na usalama.

Dk. Gwajima alisema serikali ilianzisha kampeni ya MZEE KWANZA yenye lengo la kumpa kipaumbele mzee katika maeneo yote ya kutoa huduma ambayo inalenga kuelimisha jamii kutambua na kuheshimu mchango wa wazee na wakati huo ikikumbusha kuwa kila mmoja ataupitia uzee.

Kuhusu matunzo kwa wazee wasio na uwezo, alisema serikali imeendelea kutoa huduma ya matunzo kwa wazee kwenye makazi 14 yenye jumla ya wazee 271, wanaume wakiwa 161 na wanawake 110.

Dk. Gwalima alisema serikali ina mpango wa kuanzisha makazi ya wazee kikanda na kutoa elimu kwa jamii ili familia ziwalee wazee wao na wale wachache watakaokosa huduma katika familia, kupata matunzo katika makazi hayo yatakayoanzishwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Wazee Taifa, Lameck Sendo, alisema vitendo vya ukatili dhidi ya wazee bado vinaendelea kujitokeza nchini kutokana na kuwapo kwa imani potofu.

Sendo alisema baadhi ya waganga wa kienyeji na tiba asilia wamekuwa chanzo cha kutokea mauaji dhidi ya wazee kutokana na kuleta hofu kwa jamii.

Mkurugenzi wa Shirika la HelpAge Tanzania, Joseph Mbasha, alisema shirika lake limekuwa likishirikiana na halmashauri 23 katika kupinga vitendo vya ukatili na manyanyaso dhidi ya wazee, kuboresha upatikanaji wa huduma za afya zilizo rafiki na bora kwa wazee.

Mbasha alisema afua nyingine zinazotekelezwa kwa kushirikiana na halmashauri ni kutoa huduma jumuishi wakati wa majanga, kuhakikisha usalama wa kipato na kuchagiza harakati za mabadiliko.

## Vikundi ufugaji nyuki vyapatiwa vifaa vya kisasa

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

WANACHAMA 200 wa vikundi vya ufugaji nyuki wa Wilaya ya Uvinza, Kata ya Buhingu, wamepatiwa vifaa vya ufugaji nyuki wa kisasa ikiwamo mizinga 300, vyenye thamani ya zaidi Sh. milioni 165 ili kujiongezea kipato.

Wanachama hao wanaotoka katika vijiji vya Katumbi, Nkonkwa, Buhingu na Mgambo wanajishughulisha na ufugaji wa nyuki, uvuvi pamoja na kilimo kama vyanzo vikuu vya mapato.

Akiongea na wanachama hao wakati wa kutoa mizinga, Mkurugenzi wa Mradi wa TUUNGANE, unaoratibiwa na Shirika la The Nature Conservancy na Pathifinder, Lukindo Hiza, alisema mizinga hiyo imetolewa kwa lengo la kuwafanya wananchi kutotegemea uvuvi na kilimo pekee kama njia ya kujiingizia kipato.

Alisema ufugaji wa nyuki una mazao makuu manne ambayo ni asali, nta, sumu pamoja na gundi ambayo yote yakiuzwa huongeza kipato cha familia.

"Gramu moja ya sumu inauzwa 20,000 na soko lake lipo nchini, kwa mwezi mmoja mfugaji anaweza kuvuna mara saba na hivyo kupata Sh. 140,000, bado hujauza mazao mengine, ni kazi nzuri ya kutengeneza ajira bila gharama kubwa," alisema Hiza.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Rashid Hamis, Mwenyekiti wa kikundi cha Mkombozi alisema ili nyuki wazaliane kwa wingi na kupta faida, wananchi hawapaswi kuchoma moto mapori kwa kuwa wataharibu virutubisho pamoja na vifaa walivyopewa kwa ajili ya ufugaji wa kisasa.

Naye Zahra Shaban kutokea kijiji cha Katumbi katani humo alisema wanachama waliopokea mizinga wanapaswa kuitunza na kutovunjika moyo hata kama imewekwa maeneo ya mbali na makazi, waendelee kufuatilia ufugaji wao ili kubaini changamoto kwa wakati na kuzitatua.

Kwa upande wake, Alex Robert, Mwenyekiti wa kikundi cha nta aliiomba serikali kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zao kwa kuwa wapo mbali zaidi ya kilometa 160 kutoka Kigoma mjini na kujikuta wakiuza asali na mazao mengine kwa bei ya hasara.

Naye Emmanuel Kitundu, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilaya aliwataka wanachama hao washirikiane kukuza uchumi wa kikundi, kaya na mtu mmoja mmoja kwa kufanya kazi kwa pamoja.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Buhingu, Ezekiel Rajab, alisema watashirikiana na serikali kudhibiti shughuli zote za kibinadamu zinazo ashiria kuharibu mazao ya nyuki ikiwamo kuchoma moto na kuharibu vyanzo vya maji.

# Kilwa watakiwa kuwa walinzi katika mradi bandari uvuvi

**Na Mbaraka Kambona,** KILWA

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, amewataka wananchi wa Wilaya ya Kilwa kujiepusha na vitendo vya kuhujumu ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati uliopangwa na kunufaisha wananchi na taifa kwa ujumla.

Telack aliyasema hayo wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya eneo la mradi wa ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa baina ya serikali na Kampuni ya ujenzi ya China Habour Engineering (CHEC), iliyofanyika wilayani Kilwa mkoani Lindi, juzi.

Alisema wakati shughuli za ujenzi wa mradi huo utakapoanza wakati wowote kuanzia sasa wanapaswa kuwa walinzi na wajiepushe na vitendo vya udokozi wa vifaa vya ujenzi wa bandari hiyo.

"Niwaombe wananchi wote tuwe walinzi wa shughuli zote zitakazofanyika katika mradi huu, asitokee mtu sasa akaanza kudokoa vifaa vya ujenzi hapa, tutachelewesha mradi huu kukamilika kwa wakati," alisema Telack.

Alisisitiza kuwa hategemei kuona mkandarasi analalamika kwamba kuna watu wanafanya vitendo vya wizi katika mradi huo, huku akiwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa wajenzi hao ili mradi huo ukamilike na manufaa yaanze kupatikana mapema kama ilivyokusudiwa.

Alisema kuwa kwa muda mrefu kazi ya uvuvi imekuwa ikiendelea wilayani humo, lakini manufaa makubwa bado hayajapatikana kutokana na uvuvi huo kuwa na vitendea kazi duni, ujenzi huo unategemea utasaidia kuinua shughuli za uvuvi na soko la samaki kutoka Kilwa litafunguka zaidi.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, alisema kuwapo kwa bandari hiyo ya uvuvi kutawezesha nchi kunufaika na fursa nyingi za uvuvi katika ukanda wa bahari kuu na itaongeza uwekezaji katika sekta ya uvuvi na kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Meneja Mkuu wa Kampuni ya ujenzi ya China Habour Engineering (CHEC), ambayo imepewa zabuni ya ujenzi wa bandari hiyo, Cheng Yongjian, aliishukuru serikali kwa kuwaamini na kuwapa kazi hiyo kuwa wataitekeleza kwa wakati na kuhakikisha ndani ya miezi 24 watakabidhi mradi huo kwa serikali ukiwa umekamilika.

Baadhi ya wananchi wa Kilwa akiwamo Adam Selemani na Rajab Abdallah, wote wavuvi, walionyesha kuwa na matumaini makubwa na mradi huo huku kwa nyakati tofauti wakisema kuwa watahakikisha wanashirikiana na wajenzi wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati na ni mategemeo yao kuwa mradi utakapokamilika utasaidia kuboresha shughuli zao kuliko ilivyo hivi sasa.



Mwalimu wa Nyuki wa Mradi wa Tuungane, Edward Kitenyi (kulia), akitoa maelezo kuhusu matumizi ya vifaa vya ufugaji wa nyuki. **PICHA: ADELA MADYANE**

# Kinamama wakutanishwa na watoto waliopoteana nao

**Na Sabato Kasika**

KINAMAMA watatu kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Mtwara na Dar es Salaam, wamekutanishwa na watoto wao ambao walipoteana kwa zaidi ya miaka 20.

Miongoni mwao ni Rehema Said wa Masasi mkoani Mtwara, aliyepoteana na mtoto Anuary Mbaraka (22) jijini Dar es Salaam mwaka 2000, wakati huo mtoto huyo akiwa na umri wa miezi mitatu.

Mwingine ni Happy Lema kutoka Hai, mkoani Kilimanjaro, aliyekutana na mtoto wake Boniface Rweumbiza (33), aliyepoteana mkoani humo toka mwaka 1994 wakati mtoto akiwa na miaka minne na nusu.

Kwa mujibu wa mama huyo, Boniface alizaliwa mwaka 1989 wilayani Hai, na alichukuliwa na baba yake mwaka 1994 kwenda mkoani Kagera na tangu wakati huo hajaonana na mtoto wake.

Semeni Selemani, mkazi wa Tabata Dar es Salaam, aliyepotezana na mtoto wake Mwita Adam (22), miaka 17 iliyopita baada ya kuchukuliwa na baba yake kwenda kuishi naye Musoma mkoani Mara.

Mama wa kijana huyo alisema, Mwita alichukuliwa na baba yake akiwa na umri wa miaka mitano na kwamba wamekuja kukutana akiwa na umri wa miaka 22 na haikuwa rahisi kumtambua.

Akizungumza jinsi kinamama hao walivyounganishwa na watoto wao, kiongozi wa kipindi cha Leo Tena cha kituo cha Clouds FM, Husna Abdul, kituo hicho kimekuwa na utaratibu wa kukutanisha familia zilizopoteana.

"Sasa ni mwaka wa tatu tangu kuanzisha utaratibu huo wa kuunganisha familia zilizopoteana, ambapo watu hupiga simu au kufika ofisini kuomba msaada wa kuonana na ndugu zao," alisema Husna.

Kiongozi huyo alisema, kwa njia hiyo, tangu waanze utaratibu huo, wameshaunganisha familia sita, wakiwamo kinamama watatu waliokutanishwa na watoto wao jijini Dar es Salaam juzi.

"Tunafanya mara moja kwa mwaka hasa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mama Duniani. Wito wetu ni kwamba na wazazi wajaribu kuepuka mambo ambayo husababisha watoto kupoteana nayo," alisema.

Rehema Said alisema, aliamua kumbwaga mtoto wake Anuary Mbaraka kwa mzazi mwenzake Mikocheni Dar es Salaam, akiwa na miezi mitatu baada ya kukosa fedha za matumizi na kurudi nyumbani kwao Masasi.

Naye Happy Lema, alisema mzazi mwenzake ambaye awali walikuwa wakisoma chuo kimoja mkoani Kilimanjaro, alichukua mtoto na kwenda naye mkoani Kagera akiamini angemrudisha, hakuonekana tena.Kwa upande wake, Semeni Seleman, alisema aliagana vizuri na mzazi mwenzake akarudi kwao Musoma na kilichompa wasiwasi ni kukaa kimya miaka mingi bila mawasiliano.

"Nilikata tamaa nidhani sitamwona tena mwanangu Mwita, lakini leo baba yake amemleta, nimefarijika sana," alisema Semen, huku mzazi mwenzake akifafanua kuwa hawezi kuficha mtoto kwa kuwa anajua ana mama yake.

# Serikali yashtuka wingi wa michango shuleni

OFISI ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema haitasita kuchukua hatua kwa shule itakayobainika kuwa na michango mingi zaidi ya iliyoidhinishwa kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza hadi cha sita.

Vilevile, imesema michango inayoendelea shuleni kwa sasa ni michango ya lishe ambayo imepata kibali cha mkuu wa wilaya baada ya kuidhinishwa na mkutano wa wazazi.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tarime Mjini (CCM), Mwita Michael.

Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kupunguza michango kwa wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza.

Akijibu swali hilo, naibu waziri huyo alisema michango hiyo ni kwa wanafunzi wote wa kidato cha kwanza mpaka cha nne. Alisema serikali kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa Mwaka 2015, iliamua kutoa elimumsingi (kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne) bila malipo.

"Azma hii ya serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambayo ina lengo la kuhakikisha watoto wote wa kitanzania wenye rika lengwa la elimumsingi wanapata elimu bila kikwazo chochote ikiwamo ada au michango," alisema.

Mbunge wa Bunda (CCM), Boniphace Getere, alisema elimu bure sasa ni hadi kidato cha sita na kuhoji kipi ambacho serikali itafanya kuondoa michango inayofikia Sh. 500,000.

"Sasa serikali itafanya nini? Ni kipi kuondoa michango ya Sh. 20,000 kidato cha kwanza hadi cha nne na Sh. 70,000 kwa kidato cha sita au michango cha kidato cha kwanza inafikia Sh. 500,000 wakati ya kidato cha sita inafikia Sh. 1,000,000, kipi kifanyike sasa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema elimu bila malipo inamaanisha wanafunzi hawalipi ile ada ya Sh. 20,000 wa kidato cha kwanza hadi cha nne na Sh. 70,000 kwa kidato cha tano na sita na huo ndiyo msimamo wa serikali wa kuhakikisha wanapata elimu bila malipo.

Kuhusu michango mingine, alisema wanajaribu kuiangalia ili isiathiri masomo ya wanafunzi na kuhakikisha wanapata elimu bora.

Katika swali la Mbunge wa Chemba (CCM), Mohamed Moni, alisema kumekuwapo na michango mingi kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano na kutolea mfano kuwa kuna mwanafunzi hana wazazi wala familia na amelazimika kutoa fedha mara nne ya ada na kuhoji nini kauli ya serikali ya kuhakikisha shule zenye michango hiyo inapungua.

Silinde, akijibu swali hilo, alisema michango yote lazima ipitishwe kwa kuzingatia mazingira yaliyoko na kama kuna shule au eneo lolote lenye michango mikubwa taarifa ipelekwe TAMISEMI ili hatua zichukuliwe.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Bajeti, Daniel Sillo, akiwasilisha maoni ya kamati hiyo kuhusu bajeti kuu ya serikali ya fedha kwa mwaka 2022/2023, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kila wilaya kupata mahakama 2025

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, amesema mkakati wa serikali ni kujenga mahakama kwenye kila tarafa ifikapo mwaka 2025.

Pinda alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Buhigwe (CCM), Kavejuru Felix.

Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kujenga Mahakama ya Mwanzo Tarafa za Manyovu na Muyama.

"Tarafa ya Manyovu ina kata 14 ambazo kijiografia zimesambaa kwa umbali mrefu, kata saba zina umbali wa kilometa kati ya 50 hadi 84 kwenda makao makuu ya tarafa, je, serikali ipo tayari kutusaidia mahakama mbili za mwanzo katika tarafa hii?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Pinda, alisema ofisi yake inafanya tathmini kwa kata zilizo mbali na huduma ya mahakama na kwamba serikali itakuwa tayari kutoa upendeleo na kuipa umuhimu unaostahili Tarafa ya Manyovu.

Hata hivyo, alisema kwa sasa serikali inafanya maboresho ya mahakama ambazo zilijengwa kwa mfumo wa zamani na chakavu.

Awali, katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Buhigwe ili wananchi wapate huduma.

Akijibu swali hilo, Pinda alisema ujenzi wa mahakama hiyo ni moja ya miradi ya mahakama inayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema kupitia programu ya maboresho ya mahakama, mkandarasi wa ujenzi wa mahakama hiyo ameshapatikana ambaye ni Lucas Construction na kukabidhiwa eneo la ujenzi mwezi Oktoba 2021.

"Kazi za ujenzi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2022," alisema.

# Polisi yatakiwa kumaliza uhalifu

JESHI la Polisi limekumbushwa kutekeleza ipasavyo majukumu yake ya msingi ambayo ni usalama wa raia na mali zao pamoja na kuchukua hatua kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya kihalifu kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, aliagiza hayo jana bungeni jijini hapo, alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mpwapwa (CCM), George Malima.

Mbunge huyo alisema vitendo vya uhalifu vimekithiri sana katika Kata ya Berege iliyoko wilayani Mpwapwa.

"Je, serikali itajenga lini kituo cha polisi ili kukabiliana na wimbi la uhalifu ambao limekuwa likiongezeka?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Sagini alikiri kuwapo kwa ongezeko la vitendo vya uhalifu hususani kwenye maeneo yanayokuwa na kuchipukia ikiwamo Wilaya ya Mpwapwa.

"Kuna kuongezeka vitendo vya uhalifu, uhalifu ni zao la jamii lakini si jambo jema... Ninachukua nafasi hii kulitaka Jeshi la Polisi mikoa na wilaya kuimarisha shughuli za usimamizi usalama wa raia na mali zao na kuchukua hatua thabiti dhidi ya vijana au watu wanaojiuhusisha na matendo ya uhalifu," aliagiza.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Dau Haji, alitaka kujua mpango wa serikali wa kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Dunga.

Akijibu swali hilo, Sagini alisema tathmini iliyofanyika imebaini kuwa Sh.milioni 43 inahitajika ili kukamilisha ujenzi wa kituo hicho kilichoko Wilaya ya Kati Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi inatafuta fedha hizo ili kumalizia ujenzi huo, ikiwa njia ya kuunga mkono juhudi za wananchi na wadau, hususani katika mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema serikali itaanza kujenga vituo ambavyo wananchi wametumia nguvu zao kuanza ujenzi.




Habari zote: Augusta Njoji , DODOMA


Ukurasa 12

Waziri Mwigulu katika bajeti inayoangaza kazi anayopewa na Rais Samia kutumikia nchi



Ukurasa 13

Filamu kufundisha Kiswahili shuleni tutafakari


Ukurasa 14

**Unataka kulima zao kitunguu? fuata njia hizi ufurahie maisha**

# BUFE

IJUMAA JUNI 17, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## RC KUNENGE:

# Baada kung'ara na korosho, Pwani sasa yasimama na ufuta kupaa zaidi

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKOA wa Pwani una mazao ya kimkakati ya biashara mawili ambayo ndiyo yanayong'arisha mkoa huo kwa upande wa kilimo ambayo ni korosho na ufuta.

Kilimo cha mazao haya kimekuwa kikibadilisha maisha ya walio wengi siku hadi siku hususani wale wanaofuata taratibu na kanuni za kilimo cha mazao hayo.

Pamoja na baadhi yao kuelezea kufanikiwa, pia Mkoa huo umeweka mikakati kuzalisha zaidi zao la korosho za daraja la kwanza iweze kuuza ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge, kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU) wamejipanga kufuatilia mashamba ya wakulima yasafishwe kwa wakati lakini pia upatikanaji wa pembejeo kwa muda kukuza uzalishaji.

Kunenge na timu yake wanaamua kuweka mikakati hiyo baada ya kubaini ongezeko la mauzo ya korosho katika msimu wa 2021/2022 ambapo tani 14,683 zilikusanywa ukilinganisha na msimu wa mwaka 2020/2021 ambao uzalishaji ulikuwa tani 7,778,235 na kwamba kwasasa daraja la kwanza limeongezeka hadi asilimia 72.

Pamoja na jitihada hizo za korosho, zao la ufuta nalo kwa sasa kutokana na hamasa inayoendelea hulimwa na wakulima wengi katika maeneo mbalimbali na liko mbioni kuongoza katika mazao ya biashara ya mkoa huo.

Mwezi huu ilianza minada ya zao la ufuta, ambayo bei za ufuta zimeonekana kuwa juu katika minada miwili iliyofanyika tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.



Meneja wa CORECU Mkoa wa Pwani Mantawela Hamisi, akizungumza kwenye mnada wa ufuta katika kijiji cha Kingoma wilaya ya Mkuranga. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

Mwenyekiti wa CORECU mkoa wa Pwani Musa Mng'eresa, anasema zao ufuta sasa linaenda kuwa zao kuu la biashara mkoani Pwani, kwani katika mnada wa kwanza mwaka huu kg moja imeuzwa kwa Sh.2,878 na mnada wa pili kg moja ikifikia Sh. 2,917.

Musa anasema bei hizo zimeonekana kuwa juu katika minada ya awali huku minada mingine ikiendelea hali inayohofiwa bei kuzidi kupanda, ukilinganisha na msimu wa mwaka 2021 ambapo ufuta uliuzwa kwa Sh.2,235 hadi 2,556. Mwenyekiti huyo anasema, serikali imetoa viuatilifu vya korosho vyenye thamani ya Sh.bilioni 20 kwa mkoa huo , hivyo ni vema na Ufuta ukafikiriwa kupatiwa katika kuboresha zao hilo.

Anasema katika minada, ufuta unaonekana kupata wanunuzi wengi kwa kila mnada kwani katika mnada wa kwanza walijitokeza 15 na mnada wa pili uliofanyika kijiji cha Kingoma Mkuranga wanunuzi 18 walijitokeza.

Musa anasema wanajivunia kufanyika mnada wa kwanza wa ufuta wilayani Mkuranga tangu kuanza kwa stakabadhi ghalani .

### DC MKURANGA ANENA

Akizungumza katika mnada uliofanyika katika kijiji cha Kingoma Wilaya ya Mkuranga, Mkuu wa Wilaya hiyo Hadija Nasri anatumia nafasi hiyo kuwatahadharisha Viongozi wa Vyama vya Ushirika (AMCOS) ambao sio waaminifu kukaa pembeni na kuwaachia wengine.

"Baadhi ya viongozi wa AMCOS sio waaminifu kwenye fedha za wakulima, kwa wale mnaolalamikiwa mjiandae, hili naomba lizingatiwe msiwacheleweshee wakulima fedha zao," anasema mkuu huyo wa wilaya.

Anatahadharisha, viongozi wanaoona hawawezi kusimamia wakulima, wanatakiwa kukaa pembeni.

"Fedha zinazowekwa kwenye kilimo zingeweza kupelekwa maeneo mengine lakini Serikali imezileta kwa wakulima ili kuwainua hivyo tufanye kazi kwa kushirikiana kufikia malengo ya kuinua kilimo" anasema

Akizungumzia upande wa usafirishaji anasema, kampuni zinazofanya kazi kwa kubagua zinazogundulika zikae pembeni na kupisha wengine kufanya kazi kwa utaratibu uliowekwa.

### WADAU WASEMA

Meneja wa CORECU Mkoa wa Pwani, Mantawela Hamis, anasema katika mkoa huo wana mazao ya kimkakati ambayo ni korosho na Ufuta na kwa sasa wako kwenye msimu wa ufuta na minada inaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali.

Hamis anasema katika mnada wa kwanza waliuza tani 2,500 kwa bei ya Sh.2,878 kwa kg na katika mnada wa pili 3,500 kwa Sh.2,917 kwa kilo. Mkurugenzi wa kampuni inayoshughulikia utunzaji wa maghala Rajabu Matata akizungumza katika ghala lililopo kijiji cha Kingoma anasema wamepokea tani 290 ambazo zimeingia kwenye mnada.

Anawaomba wanunuzi kuzingatia utaratibu wa stakabadhi ghalani na kuacha tabia ya kwenda kununua ufuta kwa wakulima kwa sababu ufuta mwingi wa mkoa huo hausomeki kama wote umeuzwa kwa njia ya mnada.

Matata anawashauri wakulima kuhakiki kilo kwenye vifungashio vyao pamoja na kuziweka kwenye hali ya usafi kwani wapo baadhi yao wanazidisha upimaji na hivyo kuwa zaidi ya zinazokusudiwa.

Sophia Kigoto msafirishaji wa kampuni ya Meruma, anasema kikwazo wanachokumbana nacho ni katika miundombinu ya barabara, kwani magari mengi yamekuwa yanakwama na kuchelewa kufika kwa wakati uliolengwa kwenye maghala.

# Waziri Mwigulu katika bajeti inayoangaza kazi anayopewa na Rais Samia kutumikia

• Yawa historia ya kumuinua CAG mstaafu kitini • Umma washangilia kukunwa panapowasha • Mkuu wa nchi safarini kumuibulia mitaji, soko

**Na Peter Orwa**

MADA sasa inayotawala inagusa bajeti ya taifa iliyowasilishwa bungeni Jumanne wiki hii. Ni mwitikio wa pamoja kuwa bajeti ya kubana matumizi, jambo linalombebesha sifa ya haraka, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Katika staili ya namna yake akifafanua bungeni itifaki zinazobebana, anarejea yote ni kwa mujibu wa maelekezo na miongozo ya bosi wake, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Msingi wa bajeti hiyo iliyowasilishwa safari hii, kisiasa inabeba tafsiri kuu ya kiserikali kokote duniani, kuwawajibikia wananchi na wakati huohuo, inajijengea kanuni za uhalali ikubalike kwa umma. Ishara za awali zimejitokeza kuwepo makofi zaidi kwa umma uliohojiwa, wakiwamo wawakilishi wao, wabunge

Kiutendaji, inatajwa ni bajeti kamilifu kwenye nadharia kuu ya kiuchumi kwamba inalenga kupunguza matumizi yasiyo ya lazima serikalini kadri inavyowezekana; kila senti itumike kumnufaisha Mtanzania wa chini, huku kukiwekwa mfumo tija wenye matarajio hayo kiuchumi.

Hilo likitumiwa katika lugha ya mtaani inaelezwa 'bajeti inatembelea humo humo wanakolilia wananchi' huku katika tafsiri ya kiuchumi iitwayo 'thamani ya fedha' (value for money) inaelekea kupatikana.

Hapo kitaaluma ndani yake kunaelezwa kuna maeneo mawili makuu; uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu, hali kadhalika pacha wake kitaaluma, fani ya Ununuzi na Ugavi. Vyote vikiwa na mapengo ya utendaji hata kusababisha upotevu mkubwa wa fedha za umma.

Yote yanaakisiwa na teknolojia ya mawasiliano ya umma, pia sheria zilizoko zinatoa majibu chanya na kunatajwa kuunda hatua mpya yenye mambo mapya ya kiutendaji, chini ya zama za uongozi wa Rais Samia.

Ni miaka mingi Wakaguzi wa Wakuu wa Hesabu za Serikali (CAGs) waliopitia kituo hicho walilalamikia mambo kadhaa ya kiutendaji yaliyopaswa kufanyiwa kazi, yakijumuisha, bajeti inayotosha kwa ofisi zao na kuboresha mifumo sahihi ya mawasiliano Tehama katika ofisi za umma.

Malalamiko mengine ni mali



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipoingia bungeni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"Imeelezwa kati ya mwaka 2017 na 2021, biashara zilizifayika kati ya nchi za Tanzania na Oman, zimefikia Dola za Marekani milioni112.3.**



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa ziarani nchini Oman, akizungumza na mwenyeji wake.

za umma hazina thamani inayolingana, bajeti ya mshahara iko juu katika hali isiyolingana na tija ya kinachozalishwa, vivyo hivyo hakuna mfumo unaorahisisha uwekezaji kitaifa, huku CAG anakwama kufikia taarifa na ofisi nyingi za umma.

Tayari Waziri Dk. Mwigulu amenena kwamba kutakuwapo mapitio mapya panapoonekana kukinzana na sheria za nchi, ili kusiwapo vikwazo katika utekelezaji wa mageuzi hayo.

Kwa mujibu wa Dk. Nchemba, hatua za kiserikali ikiwemo 'kuwatumbua; viongozi wa kiserikali, malipo yao yatarejea ngazi ya chini penye vyeo vya zamani, matumizi ya magari ya serikali bajeti yake kushuka kutoka wastani Sh. bilioni 550 hadi Sh. bilioni 50, wanaostahili kukopeshwa stahiki hizo ili wajigharamie.

Hayo yanatokea, huku Waziri Dk. Nchemba katika ufafanuzi wake bungeni siku kadhaa kabla, amesema matumizi ya elimu bure.

Pia, anataja mishahara ya watumishi wa umma imo katika orodha ya mambo 10 yanayochukua wastani zaidi ya asilimia 80 ya matumizi ya serikali katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Katika hatua yake kupitia uwasilisho wa serikali bungeni Jumanne iliyopita, Dk. Nchemba ametaja maeneo ambako maelekezo hayo ya Rais Samia yanaangukia, ni kuboresha na kuiwezesha Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Katika hilo anaweka bayana namna CAG atakavyopewa pesa za kutosha kama anavyoomba na kufanikisha majukumu yake.

Kwa mujibu wa Waziri Dk. Nchemba, CAG atapatiwa wataaluma kumsaidia kufanya ukaguzi kiufundi kama vile timu ya kutosha ya watumishi, wakiwamo wataalamu wa kiufundi kama wafamasia na wahandisi kusaidia tathmini na ukaguzi katika kazi zao na Tehama bora inayoleta tija kikazi.

### CAG UTOUH ACHEKELEA

Ni hoja zilizomuinua kitini CAG mstaafu Ludovick Utuoh, anayeshangilia kwa kauli: "Niseme kuwa nimefurahi sana na jana nimekunywa divai kusherehekea bajeti hii kwa sababu wakati mwingine utaratibu wa uendeshaji wa serikali unakuwa ni sababu yenyewe ya kuongeza gharama za uendeshaji wa serikali."

Anaendelea: "Kama utakumbuka wakati Rais (Samia Suluhu Hassan) anapokea ripoti ya CAG Machi 30 mwaka huu, alizungumzia na kushauri kwamba mfumo mzima wa ukaguzi wa ndani uangaliwe.

"Waziri (Dk. Mwigulu) alisema Mkaguzi wa Ndani apewe fungu na serikali inaangalia mfumo mzima wa yeye aweze kuwa na matokeo chanya zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma," anasema, pia kutoa ufafanuzi:

"Hili suala lilianza kuzungumzwa tangu bungeni kwa madereva wanakaa kwenye magari na kiyoyozi kikiwa kimewashwa kuanzia saa mbili mpaka saa sita usiku ni matumizi makubwa ya petroli.

"Fikiria hali ya petroli kwa sasa ilivyo kubwa, ile kwamba serikali imekemea kwa kusema huo utaratibu usitishwe mara moja, ni kitu kizuri sana."

### RAIS NA UWEKEZAJI

Ikiangaliwa kwa kina mstari ulipitiwa katika mfumo mpya wa uchumi na uwekezaji wake, kuna mambo kadhaa ambayo yanamrejesha mtu katika yaliyofanywa katika zama za uongozi wa muasisi wa nchi, Mwalimu Julius Nyerere.

Ni zama hizo ambazo "Kilimo ni Uti wa Mgongo' lilikuwa kipaumbele na "Elimu ni Ufunguo wa Maisha'. Katika awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi ni kwa muda mrefu fungu la elimu lilichukua wastani asilimia 20 wa bajeti ya nchi, huku ndani ya kilimo kuna mengi yamechukua nafasi.

Vipaumble vya kibajeti katika awamu iliyoko ya uongozi nchini chini ya Rais Samia, inajulikana sekta elimu hadi bajeti inayoishia, imo katika vipaumbele 10 kitaifa.

Pia, kwenye bajeti ijayo imeshawekwa bayana, ikiwemo jipya la elimu bure kwa sekondari vidato vya tano na sita, huku wanaendelea kwa elimu ya juu, kikwazo cha mikopo, kila kijana wa Kitanzania anakuwa mnufaika.

Hiyo inaendana na mapinduzi katika bajeti ijayo ya kilimo, ikiwa na nyongeza ya asilimia 155.34 kwa maana ya kutoka Sh.bilioni 294 hadi bilioni 751.23 kulenga mapinduzi ya utafiti, ruzuku ya mbolea, mbegu, kukiwapo matarajio bora kwenye uzalishaji mazao kama alizeti na ngano.

Hapo kunashuhudiwa, uhamasishaji wa kilimo ikiunganisha na uhamasishaji viwanda vya ndani vya mafuta ya kula na sukari, ambavyo malighafi yake inatoka kwenye kilimo shambani. Matokeo yake ni kukuza uzalishaji shambani, kwa namna ambayo wachumi wanaiita 'backward and forward linkage.'

Wakati kuna hatua hizo za kiserikali zinaendelea bungeni, Rais Samia amekuwa katika ziara ya kikazi nchini Oman ambako amepanua milango ya uwekezaji na biashara nchini, katika maeneo kama ya utalii,kilimo, uvuvi, ujenzi na miundombinu nchini.

Rais amewaambia wenyeji wake, namna fursa ya kufanya uwekezaji na biashara nchini inawafungulia mlango mpana wa soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Kwa mujibu wa Rais Samia, hadi sasa kuna wastani wa miradi zaidi ya 60 kutoka Oman, iliyosajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), ambayo ina thamani ya Dola za Marekani zaidi ya milioni 300 na jumla ya ajira zisizopungua 2400.

Rais Samia akiwa nchini Oman, ameshuhdia kutiwa saini hati ya makubaliano kadhaa kati ya serikali za Tanzania na Oman na nyingine kadhaa zinazohusu sekta binafsi.

Baadhi yake zinahusu makubaliano ya uendelezaji Kiwanja Cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO) na cha nchini Oman, vivvyo hivyo kuhusu maeneo ya Mamalka ya Ukuzaji Rasilimali Zanzibar (ZIPA) na Mamlaka ya Raslimali Oman.

Imeelezwa kati ya mwaka 2017 na 2021, biashara zilizifayika kati ya nchi za Tanzania na Oman, zimefikia Dola za Marekani milioni112.3.

Kwa marejeo ya hatua zinazochukuliwa kitaifa ndani ya mwelekeo wa kibajeti nchini uliotangazwa wiki hii na matukio nje ya bajeti, inafungua biashara kitaifa na kimataifa na, nguvu za uzalishaji kuanzia ngazi ya malighafi na chakula shambani.

Kimsingi, ni hatua inayosonga hadi kwenye bidhaa za viwandani na mengine yanayosafishwa sokoni, ikiwemo nje ya nchi, kutanua wigo wa soko kimataifa, Rais Samia akiwa mstari wa mbele kufungua soko, kuanzia kwenye jumuiya iliko ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), hata nje ya hapo kimataifa.

Maana yake ni nini? Uchumi na soko unakuwa, pato la taifa linaongezeka na la faraja zaidi, ajira inaongezeka kwa vijana wa kitanzania,ambao nchi yao sasa iko kwenye uchumi wa kati.

## TAFAKURI YA MLALAHOI




# Filamu kufundisha Kiswahili?



NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

TULIFUNDISHWA shuleni kwamba elimu ni mchakato wa kuhamisha maarifa kutoka sehemu moja kupeleka nyingine. Lakini kwa kifupi, ni kurithishana maarifa baina ya mtu na mtu.

Pia kuna usemi kuwa elimu ni bahari, ukimaanisha kwamba elimu haina mwisho haina ukomo, unaweza kuitafuta ukaipata hata ukiwa na umri wa kutembelea mkongojo. Ndiyo sababu tunaona wanafunzi watoto kwa wakubwa, vijana kwa wazee.

Ukitafakari sana, utaona kuwa elimu ni zana muhimu katika ukombozi wa fikra na mazingira. Na ndiyo sababu unatakiwa uangalifu mkubwa katika utoaji wake kwa binadamu, ili isije kugeuka sumu.

Kimsingi basi, elimu inaanzisha vita dhidi ya ujinga kwa binadamu, inaanzia kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kufuatiwa na stadi zingine zisizo na ukomo. Apataye elimu kwa kiwango kikubwa huitwa msomi au mtaalamu.

Huko nyuma alipata kutokea Waziri aliyeongozwa na halmashauri yake ya kichwa na kuleta mabadiliko ya kufuta michezo shuleni, akifikiria kuwa kufanya hivyo kutawafanya wanafunzi wajikite katika kusoma, kuandika na kuhesabu tu na kuona michezo ni kupoteza wakati.

Ilishangaza kuwa ilikubalika na Waziri akaendelea kulitekeleza, akisahau kuwa ni katika shule ndipo tuliwapata wanariadha kama Mwinga Mwanjala, na wanamichezo wengine mbalimbali tuliposhindanisha shule na vyuo.

Alipita akaja mwingine, akarejesha michezo na nchi ikafunguka tena katika medani ya michezo, kwa kupata vijana chipukizi katika fani hiyo na nchi kung'ara tena. Ulikuwa ni uamuzi wa mtu mmoja tu na ikawa. Sijui tulikuwa tunafikiria nini!

Nakumbuka pia, wakati fulani katika kuthamini nyimbo za wanamuziki wetu, kuna wimbo uliojulikana kama Mwanameka ukiimbwa na mwanamuziki nguli Marijani Rajab na bendi yake ya Dar International, ulikubalika kutumiwa kwenye mafunzo shuleni. Ulifikia ukatumika kutungia mitihani.

Hakukuwa na hiyana ya kutoutumia, kwa sababu maneno yake yalikuwa yanaelimisha, lakini pia yenye staha. Sina uhakika kama nyimbo za wanamuziki wetu wa leo wa Bongo Fleva au hata wasanii wa filamu za Bongo Movie, tunaweza kuzitumia kwenye mitihani au taaluma.

Lakini wakati najiuliza hayo, hivi majuzi nikasikia kuna filamu inaitwa Vuta N'kuvute, itaanza kutumika kufundisha lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari, ikielezwa kuwa itakuwa inaakisi riwaya ya Vuta N'kuvute. Nakiri sijaisoma riwaya hiyo wala kuiona filamu husika.

Kilichonishitua, ni kwamba eti mwandaaji wa filamu ndiye mtoa tamko kuwa siku za hivi karibuni filamu hiyo itaanza kutumiwa shuleni kufundisha Kiswahili ngazi ya sekondari na itatumika kujibu mitihani.

Nilishituka, kwani nilitarajia tamko zito kama hilo litolewe na Waziri mwenye dhamana ya elimu nchini na wala si mwandaaji filamu ambaye sijui na sina uhakika kama anaijua vizuri tasnia ya elimu hususan kwa sekondari.

Nikashituka zaidi kuwa tamko linatolewa mbele ya waziri mwenye dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo naye anakubali kusaidia wasanii na wabunifu, bila shaka akiunga mkono kauli ya waandaaji wa filamu.

Sipingi uamuzi huo, lakini najaribu kutafakari kama tamko hilo lilitolewa kwa wakati mwafaka na muktadha kubalika au ilikuwa ni furahisha genge, kwani walikuwa kwenye hafla! Kama ni furahisha genge basi sina neno, lakini kama imedhamiriwa, kuna la kufikiria.

Kuingiza mambo katika mtaala wa elimu ya nchi hii isiwe ghafla, wakati wanazuoni wamejifungia wakitafakari nini cha kuifanyia elimu wakati huu ambao inatolewa bila kuendana na mustakabali wa wapokeaji. Watu wanasoma wanahitimu, lakini wanarejea majumbani kana kwamba hawakuwa masomoni. Tukiingiza na Bongo Movie hapo, tutavuna mabua sasa hivi. Tuwe macho, Alamsiki!

BIASHARA

# Unataka kulima zao kitunguu? fuata njia hizi ufurahie maisha

**Na Halfani Chusi**

KITUNGUU maji ni miongoni mwa mazao yanayotajwa kuwa na kipato kikubwa zaidi na zao hilo linalotajwa kuwa kati ya mazao yanayolimwa kwa ufasaha na kuzingatia vigezo vyote vya kilimo, hata kuweza 'kumtoa' mkulima kimaisha.

Pindi mtu anapotaka kulima na kukadiria mavuno pamoja na bei kwa shamba la ukubwa wa ekari moja. Kutumia uzoefu wa kulima kitunguu, kiungo muhimu zaidi katika mboga wapishi wakisema 'bora mboga ikose nyanya lakini sio kitunguu.'

Ni kauli pekee inayotosha kukifanya kitunguu kuwa adimu kila uchwao katika masoko na hali hiyo hufanya kiuzwe kwa gharama kubwa zaidi ndani na nje ya nchi.

**SHAMBANI KUKOJE?**

Kitunguu ni muhimu na adimu na ili ukutane na pesa hizo za kitunguu, hulimwa kwa njia za kufuata kanuni zake kupata mazao bora.

Ili kulima kitunguu kwa ufasaha kwa lengo la kupata kipato bora na kujivunia mavuno, kuna mambo kadhaa kufikia mavuno mengi zaidi, mfano wa ekari moja ya kitunguu.

Kwanza kinastawi zaidi katika hali ya hewa ya baridi na inakupasa kupata ardhi yenye asili ya tifutifu kidogo, ambayo haipo katika hali ya mfinyanzi.

Baada ya hapo, unatakiwa kuweka mbegu ya kitunguu mpaka itakapofikia kupelekwa shamba inaweza kuchukua siku 25 hadi 30), kabla ya kuipeleka shambani maana upandaji wake ni kama unavyopandwa mpunga.

Kwa ekari moja mlimaji akiwa na jaruba 30, ambayo kiasi cha punje ni lita moja na nusu za mbegu, zinaweza kupanda shamba la ukubwa wa ekari moja, lakini angalizo wakati wa kuandaa mbegu inatakiwa itibiwe kwa dawa kuzuia ukungu, kutu pamoja na wadudu kabla ya kuipeleka shamba kwa ajili ya kupanda kitunguu.

Shamba la kitunguu likishakuwa limelimwa na trekta au ng'ombe kwa kadirio la ekari moja na trekta ni Sh 50,000 na ng'ombe ni elfu 50, 000 mkoani Iringa na baada ya hapo, zitaandaliwa jaruba katika ekari moja, inatakiwa kuwe na jaruba 350, ambayo kila jaruba ni Sh. 500 kulitengeneza.

Baada ya kutengeneza jaruba utafungulia maji cha kuzingatia hapo jaruba ulizozitengeneza uhakikishe unapofungulia kwa ajili ya kuja kupanda kitunguu hazivujishi maji hata tone, maana yake kingo za maji kwenye jaruba zinatakiwa kuwa na uimara mkubwa.



Mkulima wa kitunguu akiwa shamba. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Hata kama gunia lingeuzwa laki moja kutokana na hali ya soko, bado mkulima atapata Sh. milioni 10, kutoa gharama za matunzo ya Sh. milioni mbili, mkulima anabaki na Sh. milioni nane faida.**



Kitunguu katika hatua ya mavuno.

Baada ya kufanikisha, sasa hilo eneo lako la heka moja litakuwa tayari kupandwa kitungu na upandaji wa kitunguu kinapandwa kama mfano wa mpunga unavyopandwa.

Hata hivyo, kwa kitunguu huwa inaachwa nafasi kidogo kwa chini wakati wa kupanda kama nchi moja na kidogo hivi ili kitunguu kitakavyoanza kujaza chini kipate nafasi ya kutanuka.

Baada ya kupanda hapo kitunguu kuna dawa za kutumia ili kukilinda kwa sababu kinakuwa kimetolewa kwenye jaruba kimekuja kwenye ardhi nyingine kwa hiyo kwa pale kitahitaji dawa ya kuzuia majani, wadudu, pamoja na joto, ili kiweze kumea na kukua kwa wakati.

Hatua hizo hapo za kitunguu zinahitaji siku 45 tu hadi kuwa tayari kuvunwa, lakini ndani ya hizo siku inatakiwa kufungulia mara kwa mara kila kinapohitaji maji, pamoja na dawa, bila ya kusahau mbolea ya kukuzia.

Inakadiriwa kuwa katika ekari moja ya kitunguu inahitaji mifuko nane ya mbolea mifuko minne kwa ajili ya kustawisha mimea na mingine mine kwa ajili ya kukuzia hiyo kwa matunzo bora zaidi.

**KUVUNA MAPATO**

Haiwezekani kuamua kulima bila kujua kipato na soko lake likoje hapo utakuwa unatwanga maji kwenye kinu.

Iko hivi! Kitunguu kwa ekari moja kama kitatunzwa vizuri kinaweza kutoa zaidi ya gunia 100 na 'ukenge' gunia 200 (ukenge ni vile vitunguu vidogo vidogo sana) . Kitunguu kwa miaka mingi kimekuwa kikiuzwa kwa bei ya juu sana ikilinganishwa na mazao mengine kama viazi, nyanya, maharage na mchele.

Kinapokuwa adimu sana sokoni gunia, kitunguu linawezeza kuuzwa hadi Sh. 300,000 na sasa chukua (300,000 x 100) idadi ya gunia 100 hapo, unaona kabisa kuna uwezekano wa kupata zaidi ya milioni 30, huku gharama za matunzo yake hazifiki hata Sh. milioni mbili, ikiwa ni faida kubwa na inapatikana haraka zaidi ndani ya miezi mitatu tangu kupandwa.

Hata kama gunia lingeuzwa laki moja kutokana na hali ya soko, bado mkulima atapata Sh. milioni 10, kutoa gharama za matunzo ya Sh. milioni mbili, mkulima anabaki na Sh. milioni nane faida. Kwa mwekezaji, si jambo dogo.

**KWANINI HAKILIMWI?**

Watu wengi wanashindwa kulima zao hilo wengi wao wanakosa mitaji ya kuweza kuendesha kilimo hicho kwa sababu kanuni ya kupata pesa ni kutoa pesa.

Wengine wanakosa ardhi kwa ajili ya uzalishaji wa zao hilo kama nilivyosema awali kitunguu hakihitaji ardhi yenye tifutifu sana kwa sababu wataalamu wanasema ardhi yenye tifutifu inaweza kuunguza kitunguu hivyo kikatoka na rangi nyeupe badala ya rangi yake.

Na wengine wanashindwa kulima, kwa sababu ya kukosa elimu. Wengine ni imani potofu tu kwamba akionekana ni mkulima kama anaonekana mtu fulani hivi wa tofauti katika jamii kitu ambacho ni mawazo dhaifu na uchache wa upeo wa kufikiri.

***• Makala hii ni kwa mujibu wa uzoefu wake mwandishi mkoani Iringa. Anapatikana kwa simu: + 255 787879707***



## HABARI DODOMA

# Waomba serikali kuwasaidia kukamilisha ujenzi wa zahanati

**Na Renatha Msungu,** BAHI

WAKAZI wa Kijiji cha Nguji, wilayani Bahi, wameiomba serikali kuwasaidia Sh. milioni 80 ili kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya na kuepusha wajawazito kujifungulia njiani kutokana na kutembea umbali mrefu.

Wakazi hao wanalazimika kutembea umbali wa kilomita saba kwa ajili ya kutafuta huduma ya afya kutokana na eneo lao kutokuwa na kituo cha afya kwa ajili ya kupata matibabu mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Zebedayo Mussa, alisema kituo hicho hadi kikamilike na kuanza kutoa huduma kinahitaji Sh. milioni 150 na toka ujenzi uanze wameshatumia Sh. milioni 70.

Mussa, alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 50 zimetoka serikalini na Sh. milioni 20 ni nguvu kazi ya wananchi pamoja na Mbunge wa Jimbo la Bahi, Keneth Noro.

Alisema, wajawazito muda mwingine wanalazimika kujifungulia njiani kutokana na kufuata huduma ya

afya mbali takribani kilomita saba kutoka kijiji cha Nguji kuelekea Mundemu.

"Tunaomba serikali na wadau mbalimbali wajitokeze kutusaidia fedha kwa ajili ya kukamilisha kituo hiko tunahitaji kikamilike ili kuwapunguzia adha wananchi ya kuifuata huduma ya afya mbali," alisema Mussa.

Alisema, kijiji hicho kina wakazi zaidi ya 2,000 ambao wote hutembea kilomita saba kwa ajili ya kutafuta huduma ya afya.

Pia, alisema kuna muda mwingine watoto wanakosa kupata chanjo mbalimbali kutokanana umbali wa kwenda kuzitafuta katika kijiji cha jirani.

Hata hivyo, alilishukuru Shirika la World Vision kutokana na kuwajengea kituo kidogo ambacho kinatumika kwa ajili ya kliniki ya watoto na wajawazito.

Kwa upande wake, Shukrani Samwel, alisema ujenzi wa kituo cha afya katika kijiji hicho utawasaidia kwa kiasi kikubwa wakazi wa eneo hilo kutotembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Mundemu, David Mfinanga, alisema kwa siku wanalazimika kupokea wagonjwa takribani 50 kutoka maeneo ya vijiji jirani ambavyo havina vituo vya afya.

Hata hivyo, alisema anaishukuru serikali kutokana na kutoa fedha za ujenzi wa kituo hicho na anaamini kikikamilika kitapunguza msongamano wa wagonjwa kwenda katika hospitali hiyo kupata huduma za afya.

# Serikali yasikiliza malalamiko 13 ya wadau wa vyombo vya usafiri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezishughulikia hoja na malalamiko 13 kutoka kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya usafirishaji nchini, baada ya wadau wa sekta hiyo nchini kuwasilisha masuala hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Katika kuimarisha ustawi wa sekta hiyo ili iweze kukuza uchumi wa taifa, Ofisi hiyo ilikutana na wadau hao kwa nyakati tofauti na kujadili namna bora ya kuzipatia ufumbuzi hoja na malalamiko hususani ya mikataba, mishahara, posho za safari. Pia, masuala ya bima ya afya, pensheni, matumizi ya speed governor, usafirishaji wa sumu, mafuta na gesi, ukaguzi wa magari na magari kuingia vituo vya mabasi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema dhamira ya serikali ni kujenga mazingira wezeshi kwa wadau wote wa sekta hiyo wakiwamo madereva na wamiliki wa vyombo vya usafirishaji.

"Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya usafirishaji nchini kwa kuhakikisha kero na changamoto zinazoikabili sekta hii zinapatiwa ufumbuzi wa haraka na wa kudumu," alisisitiza Katambi.

Alisema hoja zote zilizowasilishwa zimefanyiwa kazi kwa kukubaliana katika vikao vya pamoja, ikiwamo viongozi wa vyama vya wamiliki wa vyombo vya usafirishaji wameahidi kutoa mikataba ya kazi kwa madereva kwa kuzingatia rasimu ya mkataba wa ajira ulioandaliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau.

Alifafanua kuwa kuhusu mishahara ya madereva kupitia benki, wamiliki wa vyombo vya usafirishaji wapo tayari kutekeleza jambo hilo.

"Aidha, serikali inawashauri madereva kufanya makubaliano na waajiri wao kuhusu suala hili kwa kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini," alisema.

Alisema serikali imewaelekeza wamiliki wa vyombo vya usafirishaji wahakikishe ifikapo Julai 30, 2022 kuwasajili wafanyakazi wao wote katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (NSSF na WCF) wakiwamo madereva.

Katambi alibainisha kuwa suala la bima ya afya kwa kuwa ni la makubaliano, wamiliki wapo tayari kukubaliana na madereva kuhusu utekelezaji wake.

Alisisitiza kuwa, matumizi ya speed governor badala ya VTS, wamiliki wana mtazamo sawa na madereva kuhusu changamoto za matumizi hayo na serikali imetoa maelekezo kwa mamlaka zinazohusika kulifanyia kazi suala hilo kwa kushirikiana na wadau wa sekta husika.

"Suala jingine lililofanyiwa kazi ni kuhusu posho za safari za ndani na nje ya nchi na mileage za safari, ambapo wamiliki wa vyombo vya usafirishaji wamepokea hoja hii.

"Na wameahidi kuendelea kufanya majadiliano ya pamoja na viongozi wa vyama vya wafanyakazi madereva na kufunga mkataba wa hali bora kwa lengo la kuboresha posho na maslahi mengine ya madereva, kwa kuzingatia utofauti uliopo baina ya mwajiri mmoja na mwingine," alisema.



Baadhi ya watoto kutoka maeneo mbalimbali nchini wakishiriki maandamano ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika Kitaifa, kwenye viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tanzania Bara, Visiwani wakubaliana ushirikiano mifugo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI ya Muungano Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zimeweka makubalianao ya kushirikikana katika sekta ya Mifugo ili kusaidiana kutatua kero mbalimbali ikiwemo soko la uhakika la mazao ya mifugo.

Kaimu Katibu Mkuu Sekta ya Mifugo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Mhina, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika kikao kilichozihusisha pande hizo mbili.

Dk. Mhina, alisema wamekubaliana kushirikiana katika mambo mbalimbali yanayohusu sekta hiyo ili kuongeza tija ya mifugo na kudhibiti magonjwa ya mifugo.

"Eneo jingine ni katika masoko ya uhakika ya mazao ya mifugo, kudhibiti magonjwa ya mifugo na kuweka mikakati ya kuinua sekta ya mifugo kwa Tanzania bara na Zanzibar," alisema Dk. Mhina.

Kadhalika, alisema katika kikao hicho wamepitia mazungumzo ya kikao kilichopita na kupata maadhimio mapya ambayo yatakwenda kujibu kero mbalimbali zilizopo katika sekta hiyo baina ya pande hizo.

"Lengo kubwa la kikao hiki ni kushirikiana katika masuala ya afya za mifugo, uzalizashaji mifugo bora, masoko ili kuwa na soko kubwa la mazao yetu ya mifugo," alisema Dk. Mhina.

Alisema katika sekta hiyo bado zipo changamoto mbalimbali ikiwamo mbegu za mifugo zisizokuwa na ubora.

"Makubaliano ya kikao hiki ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na mbegu bora za mifugo ambazo zitaongeza tija katika sekta hii kwa kubadilisha uzoefu baina ya Zanzibar na sisi Tanzania Bara," alisema Dk. Mhina.

Pia, alisema eneo jingine ambalo wanakwenda kushirikiana ni uzalishaji wa malisho ambayo imekuwa moja ya kero kwa sekta hiyo nchini.

Alisema, wanakwenda kuanzisha utaratibu wa kutoa mbegu kwa ajili ya malisho ya mifugo ili kukabili kero hiyo wafugaji kwa muda mrefu.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Asha Zahara Mohamed, alisema lengo la kikao hicho ni kujadili changamoto zinazaokabili sekta ya mifugo kwa serikali zote mbili na kuzitafutia suluhu.

"Katika kikao hiki tumejadili changamoto ya magonjwa ya mifugo yale ambayo yanavuka mipaka, kuboresha mifugo yetu, malisho na kushirikiana katika tafiti mbalimbali na mafunzo," alisema.

Vilevile, alisema Zanzibar bado inakabiliwa na tatizo la chakula cha mifugo, malisho, dawa za mifugo hivyo kufanya bei ya mazao ya mifugo kuwa kubwa ikilinganaishwa na Tanzania Bara.





# Mbaroni kwa kujifanya mkuu wa mkoa Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Warren Mwinuka (20), mkazi wa Mtaa wa Makondeko, jijini hapo kwa tuhuma za kujifanya mkuu wa mkoa wa Mbeya, akitumia akaunti ya mtandao wa kijamii wa Instagram kuwatapeli watu ili awatatulie kero mbalimbali zinazowakabili.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, mtuhumiwa huyo alikamatwa Juni 7, majira ya saa nane mchana katika eneo la Mama John, alipokuwa akiendelea kuwatapeli watu kupitia akaunti hiyo feki.

Alisema mtuhumiwa huyo alikuwa akitumia akaunti ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, kuwahadaa wananchi na kutoa namba yake ya simu ili mtu au watu kupeleka kero na s hida mbalimbali kwake azitatue.

Alisema baada ya Jeshi la Polisi kumkamata, alikiri kufanya udukuzi huo na aliamua kufanya hivyo kwa sababu ya kumpenda mkuu huyo wa mkoa.

Aliongeza kuwa upelelezi wa shauri hiyo unaendelea na baada ya kukamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani na kwa mujibu wa sheria anaweza kufungwa jela miaka mitatu, kulipa shilingi milioni tano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

"Nawatahadharisha wananchi kufungua akaunti feki ya mtu na kujifanya wewe ndiye kiongozi au taasisi fulani kwa lengo la kufanya vitendo vya uhalifu ni kosa kwa sheria za mitandao ya kijamii natoa rai kwa Watanzania kuachana na utapeli kwa namna hiyo ili kujiepusha na mkono wa sheria," alisema Matei.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema ni akaunti nyingi feki zimefunguliwa kupitia ukurasa wake wa Instagram na kwamba yeye pamoja na wataalamu wake wameshindwa kuifuta.

Alisema kijana Mwinuka aliifungua akaunti hiyo kwa utaalamu hali iliyowafanya kushindwa kuifuta na wanaendelea kufanya jitihada za kuiondoa.

Homera aliwaasa viongozi wenzake kujenga tabia ya kukagua na kujiridhisha na akaunti zao za mitandao yote ya kijamii ili kuepukana kuchafuliwa kwa kuwa ni gharama ya kufuta doa hilo kubwa hadi kujulikana kwamba sio mhusika itachukua muda mrefu.

"Mwinuka alikuwa anahamisha taarifa na habari mbalimbali kutoka kwenye akaunti rasmi ya Mkuu wa Mkoa kuweka kwenye akaunti feki ya kwake huku akitumia picha mbalimbali za viongozi wa nchi," alisema Homera.

Alisema Mwinuka alikuwa akitumia akaunti hiyo kuwalaghai watu kwamba yeye ndiye mkuu wa mkoa na anapokea na kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wananchi, licha ya kuwa hadi anatiwa nguvuni hakuna mtu yeyote aliyemtapeli.

Mwinuka, alikiri kufanya kosa hilo na kumwomba msamaha mkuu wa mkoa na kueleza sababu ya kufanya hivyo ni upendo wake kwake.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (watatu kushoto), akipokea msaada wa vifaa vya kutunza taka kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori, wakati benki hiyo, ilipokabidhi vifaa 100 vyenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya mkoa huo, jana. Katikati ni Katibu Tawala mkoa huo, Dk. Fatma Mganga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vijana 178 wapatiwa mikopo ya bodaboda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust, inayojishughulisha na uwezeshaji wananchi kiuchumi, imetoa mikopo ya pikipiki kwa vijana 178 kuwawezesha kujiajiri na kujikwamua kiuchumi kupitia biashara hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Meneja wa Taasisi hiyo, Jackline Boaz, alipokuwa akikabidhi pikipiki sita zenye thamani ya Sh. milioni 19.2 kwa chama cha madereva bodaboda jijini hapo ikiwa ni mikopo kwa vijana.

Alisema mikopo hiyo imelenga kutekeleza mikakati ya kuwezesha wajasiriamali na vijana kiuchumi kupitia Mkurugenzi wa Taasisi ya Tulia Trust ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya na Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson.

"Kama ilivyo kawaida kwa Spika kuwezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mikopo ya pikipiki na bajaji kwa lengo la kuwawezesha vijana kuachana na matukio ya uhalifu na kujiajiri na kutoa ajira kwa wengine," alisema.

Mwenyekiti wa Bodaboda Jiji la Mbeya, Aliko Fwanda, alisema kuwa mikopo hiyo imekuwa na tija kubwa kwa vijana kujiajiri na kurejesha kwa wakati pasipo usumbufu na kubainisha kuwapo kwa riba ya asilimia mbili.

Dereva bodaboda aliyenufaika na mkopo, Kelvin Patrick, alisema kuwa mikopo imetoa fursa na kuachana na matukio mbalimbali ya uvunjifu wa sheria za nchi na kumshukuru Dk. Tulia kwa kuokoa kundi kubwa la vijana.

**"Kama ilivyo kawaida kwa Spika kuwezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mikopo ya pikipiki na bajaji kwa lengo la kuwawezesha..**

# Mfumo utoaji vibali kielektroniki wazinduliwa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imezindua mfumo mpya wa utoaji vibali kielektroniki kusafirisha mifugo na bidhaa zote zitokanazo na ngozi ili kuondoa urasimu, rushwa na uzembe uliokuwa unafanywa na baadhi ya wataalamu wanaoshughulikia upatikanaji wa vibali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Tixon Nzunda, alisema jana kuwa mfumo huo utaanza kutumika rasmi Julai mosi, mwaka huu.

Alisema mfumo huo utarahisisha shughuli za utoaji vibali kwa njia ya mtandao na wafanyabiashara hawatapanga foleni kwa wataalamu wakiwamo maofisa ugani kushughulikia vibali vya kusafirisha mifugo na mazao yatokanayo na mifugo badala yake watatumia teknolojia za simu na kompyuta kuvipata.

Alisema serikali ilianzisha mfumo huo kuokoa na kukusanya mapato yatokanayo na ukataji wa vibali na kuwabana watumishi waliokuwa wakiendekeza rushwa na urasimu kuwahudumia wananchi.

"Tunajivunia kuona sasa tumefanikiwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki ambao utatumika kutoa vibali vya usafirishaji wa mifugo na bidhaa zake, kama vile ngozi, mayai na nyama kutoka kila pembe ya nchi huko aliko atapata kibali chake kupitia simu yake ya mkononi na kuendelea na shughuli zake," alisema Nzunda.

Alisema wameamua kuutambulisha mfumo huo kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hususani mkoani Mbeya kwa kuwa ni eneo ambalo linawafugaji wengi ambao wanafuga kisasa na kuzalisha maziwa yenye ubora unaokubalika kimataifa.

Kwa upande wake, Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Daniel Mushi, alisema mfumo huo utawarahisishia wafanyabiashara wa nyama nchini kupata vibali kwa wakati na kufanya shughuli zao kwa uhuru. Alisema mfumo huo utapunguza mlolongo mrefu wa kufuatilia vibali katika ofisi za serikali na badala yake vitakatwa kielektroniki.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Trade Mark East Afrik, Lilian Masalu, alisema walishawishika kuisaidia serikali kuanzisha mfumo huo baada ya kuona ucheleweshwaji wa vibali vya kusafirisha mifugo hali iliyokuwa inasababisha bidhaa zitokanazo na mifugo kuharibika na wafanyabiashara kuingia hasara.

Alisema mfumo huo utakuwa na tija kwa mfugaji na mfanyabiashara ambao kwa pamoja watauza kwa wakati na kujiingizia kipato.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaojishughulisha na uuzaji wa ngozi walisema mfumo huo utasaidia kuwa na bei ya pamoja nchini kuliko ilivyo sasa.





Mnufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Bahati Vuai Haji, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), waliofika katika eneo lake la biashara ya mgahawa wa chakula, katika kijiji cha Kwareni, Vitongoji Pemba jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanufaika TASAF watoa ushuhuda wa mafanikio

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANUFAIKA wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) kisiwani Pemba wamesema miradi waliyoibua imewakomboa kiuchumi na kumudu gharama za kusomesha watoto wao shule.

Wamesema miradi mingi waliyoianzisha kutokana na ruzuku wanazopokea kupitia mpango huo, imewatoa kwenye umaskini na sasa wana uhakika wa kupata kipato cha kujikimu kimaisha.

Wanufaika hao waliyasema hayo wakati wakizungumza na waandishi wa habari katika ziara ya maofisa wa TASAF waliowatembelea juzi.

Mnufaika Bahati Vuai Haji wa Kijiji cha Kwareni Vitongoji, Mkoa wa Kaskazini Pemba aliyeanzisha biashara ya mgahawa, alisema kuwa kabla ya kuwezeshwa na TASAF, hali yake kiuchumi ilikuwa ngumu.

Alisema baada ya kupatiwa ruzuku hiyo, aliweka akiba na kuanzisha biashara ya bagia na kujiunga katika vikundi vya kuweka na kukopa na ndipo alipoanzisha mgahawa wa chakula ambao sasa unaiendesha familia yake yenye watoto watano.

"Ninashukuru hivi sasa napata fedha, familia yangu inapata huduma mbalimbali ikiwamo ya chakula. Kabla ya kupatiwa ruzuku hii, nilikuwa ninapata shida kuwahudumia watoto wangu kwa sababu baba yao hana msaada wowote," alisema.

Bahati alitaja mafanikio aliyopata ni kununua kiwanja, kusomesha watoto wake na kuilisha familia angalau milo miwili tofauti na ilivyokuwa awali.

Mnufaika huyo alisema bado mtaji wake ni mdogo, hivyo anahitaji fedha kwa ajili ya kuboresha biashara ili huduma anayoitoa kwa wateja wake iwe na ubora zaidi.

Mnufaika mwingine, Saumu Amour Muhammed, Mkazi wa Kijiji hicho, alisema kuwa baada ya kupata ruzuku ya Sh. 84,000 kutoka TASAF, alianza kufanya biashara ndogo na kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa na faida aliyoipata akaiwekeza katika kilimo cha mboga na matunda.

Alitumia fursa hiyo kuiomba serikali kuendelea kuwapatia elimu na mitaji itakayowawezesha kukuza biashara zao na kutoa ajira kwa wengine.

# Wenye ualbino walia na vikwazo

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

LICHA ya juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na serikali na taasisi mbalimbali za kupigania haki za watu wenye ualbino, bado kundi hilo linakumbwa na matatizo ya kimaumbile na kimazingira na kushindwa kutimiza ndoto zao.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watu Wenye Ualbino, Yussra Mmanga, alibainisha hayo jana wakati akikabidhi ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja huko Tunguu vifaa vya kulisaidia kundi hilo.

Alisema kundi kubwa la watu wenye ualbino bado liko nyuma kiafya, kijamii na kielimu kwa kuwa mazingira ya kupatiwa elimu hayako rafiki kwao.

Mmanga alisema kundi hilo lina matatizo ya uono hafifu na kuiomba serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuangalia uwezekano ya kuwaandalia mazingira yatakayowawezesha kukabiliana vyema na hali zao ikiwamo kuwachapishia vitabu maluum vyenye maandishi makubwa ili kusoma kwa urahisi.

"Tunahitaji vitavu vyenye maandishi makubwa kutokana na tatizo tulilonalo la uoni hafifu ili tuweze kufanya vizuri katika masomo yetu na kufaulu katika mitihani ya taifa," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema umefika wakati serikali kuchukua juhudi za makusudi za kuwaelimisha walimu kutoa ushirikiano kwa watu wa aina hiyo wakati wanapofundisha shuleni ili nao washiriki kikamilifu kupata elimu kama wanavyopata wanafunzi wengine.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema serikali itahakikisha inakuwa karibu na watu wenye ulemavu ili wapate haki zao zote za msingi ikiwamo elimu.

"Suala la elimu linahitaji kupatiwa watu wote bila ya ubaguzi kwa sababu watu wenye ulemavu wana haki sawa kama watu wengine wasio na ulemavu," alisisitiza.

Katibu wa Watu Wenye Ualbino Wilaya ya Kati Unguja, Kazija Juma Abdalla , alishukuru jumuiya hiyo kwa msaada huo uliojumuisha mafuta maalum ya kukabili mionzi ya jua, ambao utasaidia kutunza afya zao na kuziomba taasisi zingine na wadau mbalimbali kuendelea kuwasaidia ili kuondokana na matatizo yanayowakabili.

# Waziri aipa angalizo CRDB utoaji mikopo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amewataka watendaji wa Benki ya CRDB kuwa makini katika utoaji wa fedha za UVIKO-19 ili kuhakikisha wanapewa watu sahihi ambao watazitumia na kuzirejesha kwa wakati.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo yaliyowashirikisha wakuu wa wilaya, mikoa, watendaji wa benki hiyo na watendaji wa wizara yake, Soraga alisema ni vyema kabla ya walengwa kupatiwa fedha hizo, wapewe mafunzo ya kuwajengea uelewa ili iwe rahisi kuzirejesha na kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema ili kufikia malengo hayo, ni muhimu kuandaliwa kwa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji na kuweka takwimu sahihi ambazo zitasaidia katika ufuatiliaji na kukuza uchumi.

Katibu Mkuu anayeshughulikia kazi na uwekezaji katika wizara hiyo, Khadija Khamis Rajabu, aliwataka washiriki wa mkutano huo kujadili kwa kina matatizo yaliyojitokeza katika utoaji wa fedha za mkopo wa UVIKO-19 ili kutoa fursa katika utekelezaji wa kazi zake.

Alisema fedha hizo ni mwendelezo wa fedha za ahueni zilizotolewa na serikali ambazo zilitolewa kwa vikundi na sasa zinatarajiwa kutolewa kwa mtu mmoja mmoja, hasa wafanyabiashara na wawekezaji.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema wako tayari kufanya kazi kwa ushirikiano ili fedha hizo ziendane na matumizi ya biashara katika maeneo husika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**AMANI PAUL**O anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0156-0121 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **TANGA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1268-0520 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KISIMIRI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015 na cheti cha chuo na transcript chenye usajili namba **2015-04-02001** kilichotolewa na **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi .

**POLISI TAARIFA: TAN/TAN/RB/582634/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 46 YA 2022**

**GERVAS N.TETI, NARCIS M.LEENGA, JOHN MORIS (msimamizi wa mirathi ya marehemu), JAMES M.MARANDU..................WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SAID RAJABU MTENGWA,MARIAM P.PAPI,SADIKI SELEMANI ZEMBWE,HASAN MATAKA,SAID R.MTANGA,JUMANNE LUGENDO,MOHAMED NASSORO,MAANGAZA RAMADHANI SUME,PAULO MTEPA ,MAMA SIMBA,MAMA FURAHA,MAMA BITE,TAUSI SELEMANI KONGOLO,CHARLES ULIME,TATU MSTAPHA,HAMISI KAMBA,ATHER MAGARA,HELANA DAMAS,JOVITA NETO,KAROLINA PAULI,LAUTELI MATHEI,SAID OMARI AMISI,ESTA DAMASI,JUMA HASAN,AMOSI MAGANZA.**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

MARIAM P.PAPI,SADIKI SELEMANI ZEMBWE, SAID R.MTANGA,JUMANNE LUGENDO,MOHAMED NASSORO,MAANGAZA RAMADHANI SUME,PAULO MTEPA ,MAMA SIMBA,MAMA FURAHA,MAMA BITE,TAUSI SELEMANI KONGOLO,CHARLES ULIME,TATU MSTAPHA,HAMISI KAMBA,ATHER MAGARA,HELANA DAMAS,JOVITA NETO,KAROLINA PAULI,LAUTELI MATHEI,SAID OMARI AMISI,ESTA DAMASI,JUMA HASAN,AMOSI MAGANZA ,Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 29/06/2022 mbele ya Mwenyekiti M.Khassim ninyi wenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 08/06/2022.

**M.KHAMISI**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

---

## UNCLE MO ENTERPRISES

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya udalali ya **UNCLE MO ENTERPRISES** kwa mamlaka iliyopewa na Mahakama ya Tanzania inatangaza nnada wa hadhara utakaofanyika tarehe 22/06/2022 kuanzia saa nne kamili asubuhi katika maeneo ya Uhindini Dodoma. **MNADA HUO NI WA KUUZA GARI AINA YA TOYOTA IST YENYE NO.ZA USAJILI T 999 BMF MALI YA NDUGU ALFRED GLADNES SIMON NB**

- Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizolipa hazitarudishwa.
- Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzingatiwa.

**WOTE MNAKARIBISHWA**
**MAWASILIANO**
**0717417520, 0717073423**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo.........PONGWE......**
**Usimamizi wa Mirathi ...27......2022...**
**Ombi la**
**VERONICA P. MAKANGE............Kuteuliwa Msimamizi Mirathi ya Marehemu ANNA P. MAKANGE............**

**Kwa YOYOTE ANAEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 4/7/2022** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 14/06/2022**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA.
Tarehe 12-04-2022

## TANGAZO

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA** tarehe **17/06/2022.** kampuni ya **LAL TRADING CO. LIMITED** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM PORT** kuelekea **AZAM MARINE** kupitia **BANDARI.**

1. Gari hizo zenye namba za usajili na vipimo vyake:
   a) **T 297 DTR/ T 848 DUL UREFU 23 UPANA 4.7 KIMO 5.2**
   b) **T 505 DDM/T 551 DLX UUREFU 23 UPANA 4.7 KIMO 5.2**

Gari hizo zinatoka **DAR ES SALAAM PORT** kuelekea **AZAM MARINE** kupitia **BANDARI.** Gari zitasafiri muda wa mchana tu (**kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka sasa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **ANATOLIA KOKWINUNURA KILAMA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Mitsubish Canter lenye namba za usajili **T350 BTF**, injini namba **4D33J54448** na chassis **FE71CB503117.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/237167/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige **simu namba 0754407697.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI DODOMA, Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 84/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SALOME HUSSEIN KONDE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ZUENA MOHAMED KILALA**

**TANGAZO**

*(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **tarehe 20 Mwezi 06 Mwaka 2022** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imtolewa leo Tarehe 15/06/2022.**

HAKIMU

PRINCIPAL ... COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**WINFRIDA LINUS SANGA,** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye index **no S.2550.0038** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya Secondary **MLONDWE Mwaka 2016.** Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa ya polisi**
**DOD/DOD/RB/238459/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......28 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: PRISCILLA NESTOR MPEKA WA BIGWA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: EPHYGENIA F. MATHEN**

**TANGAZO**

***(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 06 Mwezi 06 Mwaka 2022**

**HAKIMU**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALLY SAID ALLY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S.2823/0029** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **GOROWA SEKONDARI** mwaka 2016. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **TAARIFA YA POLISI: DSM/PHQ/RB/236277/2022.**

---


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Kenya yataka wanajeshi kutumwa DRC

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya Uhuru Kenyatta, ametoa wito wa kutumwa haraka kwa kikosi cha kanda ya Afrika Mashariki ili kurejesha usalama katika maeneo yenye matatizo ya mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Katika taarifa yake, alitoa wito wa kusitishwa mara moja kwa uhasama wote kwa makundi yote yenye silaha, ya kigeni na ya ndani, kuweka silaha chini mara moja na bila masharti.

Jeshi la Kanda ya Afrika Mashariki, litatumwa mara moja katika mikoa ya Ituri, Kivu Kaskazini na Kusini ili kulinda amani kwa kushirikiana na vikosi vya Umoja wa Mataifa (Monusco).

Alisema uamuzi wa kuanzisha kikosi cha kikanda ulifanyika Aprili wakati Kenyatta, mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, alipokutana na viongozi wenzake kuzungumzia kuhusu mgogoro wa DR Congo ambao pia unatishia nchi jirani.

Zaidi ya vikundi 100 vya ndani na nje vinafanya kazi katika majimbo ya Kivu Kusini, Kivu Kaskazini na Ituri na vimevuruga eneo hilo kwa zaidi ya miongo miwili.

Tangu mwezi Machi, mapigano kati ya jeshi la Congo na waasi wa M23 yamewakosesha makazi zaidi ya watu 80,000.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imeishutumu Rwanda kwa kuunga mkono kundi linaloundwa na Watutsi wa asili ya Congo, lakini serikali ya Kigali inakanusha tuhuma hizo.

Katika hatua nyingine, kikao cha baraza la usalama la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kimeiomba serikali kusitisha makubaliano na itifaki zote ambazo nchi hiyo inazo na Rwanda kutokana na madai ya kuvamiwa na kuunga mkono waasi wa M23.

Hata hivyo, Rwanda mara kwa mara imekanusha kuhusika katika mgogoro unaoendelea nchini DR Congo.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na mkutano wa usalama uliofanyika Jumatano jioni ukiongozwa na Rais Felix Tshisekedi, ulitoa ombi kwa Rwanda kuondoa mara moja wanajeshi wake chini ya kundi la kigaidi la M23 kutoka eneo la Congo.

Huko Rutshuru, jimbo la Kivu Kaskazini, ambapo M23 wanakalia mji wa mpaka wa Bunagana tangu Jumatatu, wenyeji wanahofia mapigano mapya na mabaya zaidi ambayo yanaweza kuanza tena wakati wowote.

Msemaji wa jeshi katika jimbo hilo, Luteni kanali Guillaume Kaiko, aliiambia BBC kwamba mahitaji yote sasa yamewekwa kwa jeshi kuukomboa mji kutoka kwa waasi.

Waasi wa M23 ambao wanasisitiza wanataka mazungumzo na serikali, walisema serikali imetuma wanajeshi kati ya 1,000 na 2,000 zaidi huko Rutshuru ambao hawajakwenda kwa amani. **DW**

# Viongozi wa Ulaya wakaribishwa na ving'ora vya tahadhari Ukraine

**KYIV,** Ukraine

MILIO ya ving'ora vya tahadhari vilisikika mjini Kyiv, nchini Ukraine, wakati viongozi wa Jumuiya ya Ulaya (EU) walipowasili.

Hata hivyo, ni jambo la kawaida katika mji huo kusikia sauti hizo, lakini ilitumika kama kuwakumbusha viongozi hao kutoka Ufaransa, Italia na Ujerumani kuwa wapo katika nchi yenye vita.

Viongozi waliowasili nchini humo kwa ajili ya mazungumzo na Rais Volodymyr Zelensky ni Emmanuel Macron, Kansela Olaf Scholz na Waziri Mkuu wa Italia Mario Draghi.

Katika ziara yao watakutana na Zelensky ili kuonyesha wanaunga mkono kwa Ukraine.

Scholz aliliambia gazeti la kila siku la Ujerumani, Bild kwamba wanataka kuonyesha sio tu mshikamano, lakini kuhakikisha wanauandaa msaada wa kifedha, kibinadamu na silaha.

Shambulio la Russia laua wanne Ukraine

**China inadai kutoegemea upande wowote, lakini tabia yake inaonyesha wazi kwamba bado inawekeza katika uhusiano wa karibu na Russia.**

Mashambulizi ya usiku kucha ya roketi zilizorushwa na ndege za Russia yalipiga kitongoji cha mji wa kaskazini mwa Ukraine wa Sumy na kuwaua watu wanne na kuwajeruhi wengine sita, Kulingana na Gavana Dmytro Zhyvytskyi, hakutaja lengo la shambulio hilo katika kitongoji hicho.

Alisema kwamba roketi nyingine ilishambulia wilaya ya Dobropillia asubuhi ya jana karibu na mpaka wa Russia.

Aliongeza kuwa shambulio hilo lilifuatiwa na mashambulizi mengine 26 kutoka mpaka wa Urusi.

**CHINA YAONYWA KUWA HATARINI**

China imejaribu kuwa na sera ya kutoegemea upande wowote katika mzozo huo, ikijaribu kutoa wito kupata suluhu kwa njia ya amani.

Rais Xi Jinping wa nchi hiyo katika taarifa yake alimhakikishia Rais Putin wa Russia kuwa anamuunga mkono kwa kutafuta uhuru na usalama wake.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, ilisema kauli hiyo imeifanya Marekani kuelezea wasiwasi wake, ikionya kwamba mataifa ambayo yanaegemea upande wa Putin katika uvamizi wake Ukraine yatakuwa upande mbaya wa historia.

"China inadai kutoegemea upande wowote, lakini tabia yake inaonyesha wazi kwamba bado inawekeza katika uhusiano wa karibu na Russia," msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Marekani alisema.

Biashara kati ya China na Russia iliongezeka katika robo ya kwanza ya mwaka, ikipanda kwa asilimia 28 kutoka mwaka uliopita, kulingana na data ya forodha ya China. **BBC**



Raia wa Msumbiji wakikimbia mapigano katika jimbo la Cabo Delgado yaliyoibuka tena hivi karibuni. **PICHA: AFP**

# 15,000 wakimbia mashambulizi

**MAPUTO,** Msumbiji

ZAIDI ya watu 15,000 wamekimbia makazi yao katika wimbi jipya la mashambulizi katika jimbo la kaskazini mwa Msumbiji la Cabo Delgado.

Kulingana na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), mashambulizi hayo yalianza takriban wiki moja iliyopita kusini mwa jimbo hilo, ambalo lilionekana kuwa salama.

Migogoro katika eneo hilo ilianza mwaka wa 2017, zaidi ya watu 4,000 wameuawa na wengine 800,000 kulazimishwa kukimbia makazi yao.

Watu wanaokimbia wengi wao ni watoto na kuna wanawake wajawazito 125.

Mashambulizi hayo mapya yapo katika maeneo yaliyo karibu kilomita 100 kutoka Pemba ambako kumekuwa kimbilio la watu wengi.

IOM ilisema kwamba watu wanatakiwa kurudi kwa hiari kutoka katika maeneo waliyokimbilia, jambo linalokinzana na msukumo wa mamlaka kuwataka watu kurejea.**BBC**

# Waliouawa kwenye shambulio wafikia 86

**OUAGADOUGOU,** Burkinafaso

IDADI ya vifo kutokana na shambulio lilofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita kaskazini mwa Burkina Faso, imeongezeka na kufikia watu 86.

Taarifa ya serikali ilisema idadi ya awali ya shambulizi hilo lilofanywa na kundi la kijihadi katika kijiji cha Seytenga, ilifikia 79.

Kiongozi wa jeshi la nchi hiyo, Paul-Henri Damiba, aliahidi hatua kali dhidi ya washambuliaji hao wakati alipotembelea eneo la mkasa.

Burkina Faso imekuwa ikikabiliana na uasi wa wanajihadi tangu mwaka 2015, na kugharimu maisha ya maelfu ya watu na wengine kukimbia makazi yao karibu milioni mbili.

Uvamizi huo ni kikwazo kwa serikali ya kijeshi, ambayo ililazimisha kuingia madarakani ikishutumu serikali iliyochaguliwa kwa kushindwa kushughulikia ukosefu wa usalama.

Mgogoro huo ambao pia unaathiri maeneo mengi ya Mali na Niger, unazifanya jamii za vijijini kuyahama makazi yao. **DW**

# TUTAENDELEA KUPAMBANA HADI MWISHO - KOCHA AZAM

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, ameonyesha kufurahishwa na vijana wake jinsi walivyopambana hadi kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya Kwanza na kuahidi kuwa wataendelea kufanya hivyo ili kumaliza kwenye nafasi tatu za juu.

Alisema hayo baada ya timu yake juzi, kuondoka na ushindi huo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ikiwa ni mechi za kuelekea kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**"Kila mechi ni ngumu na ina ushindani, tumepata pointi tatu nawashukuru vijana wangu kwa kupambana hadi kupata ushindi kwa sababu haikuwa rahisi, najua tutaendelea kushinda ili kuwa kwenye nafasi za juu," alisema.**


"Sijaridhika kwa sababu msimu huu haukuwa mzuri kwetu, lakini najivunia kuwa tayari kuna baadhi ya vitu vimeshaanza kurekebishika ikiwamo kutoruhusu mabao, kwenye mechi ya nusu fainali hatukuruhusu bao, tumefungwa kwa mikwaju wa penalti na mechi hii pia kutoruhusu bao lolote, ina maana kuna kitu kimeongozeka, ingawa bado naendelea kukisuka kikosi."

Ni matokeo ambayo yanaifanya Azam kurejea kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi 40, ikiishusha Geita Gold kwenye nafasi ya nne na pointi zake 39.

Azam inaisaka nafasi ya tatu kwa udi na uvumba ambayo itaifanya kurejea kwenye michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika, baada ya msimu uliopita kuambulia patupu, huku pia ikiikosa nafasi hiyo kwa kutolewa na Coastal Union kwenye Kombe la FA.



Makamu wa Rais wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Henry Tandau (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu kamati hiyo kupata msaada wa mazoezi ya olimpiki kwa wachezaji watano watakaoshiriki Olimpiki mwaka 2024 nchini Ufaransa. Kulia ni Katibu Mkuu wa Kamati hiyo, Flbert Bayi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# Pluijm atajwa Singida Big

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Singida Big Stars uko katika mchakato wa kumchukua Kocha Mkuu wa zamani wa Yanga, Hans van der Pluijm ili kukinoa kikosi hicho kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Singida Big Stars zamani ilikuwa DTB FC imepanda na kucheza Ligi Kuu msimu ujao na kuhakikisha wanaboresha kikosi chao kwa ajili ya ushindani mkubwa kwa msimu huu.

Taarifa za uhakika zilizofikia gazeti hili jana kutoka kwa mmoja wa viongozi wa Singida Big Stars ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema wako katika mazungumzo na Pluijm huku msaidizi wake akitajwa kuwa mwalimu wa Mbeya City, Mathias Lule.

Alisema muda wowote Pluijm na Lule wanatarajiwa kujiunga na kikosi hicho kwa sababu mazungumzo na makocha hao yalishaanza muda mrefu na bado yanaendelea.

"Tunatakiwa kuimarisha kikosi chetu, lakini kwanza tuboreshe benchi la ufundi kwa kuleta kocha mpya, lakini pia tumeanza kufanya usajili wa baadhi ya wachezaji wapya," alisema kigogo huyo.

"Tayari tumeshamalizana na wachezaji saba ambao wamesaini mkataba wa miaka miwili ambao ni golikipa wa Polisi Tanzania, Metacha Mnata, beki wa KMC FC, Andrew Vicent 'Dante', Abdul- Majid Mangalo kutoka Biashara United," alisema kigogo huyo.

Aliwataja wengine ni beki wa Simba, Michael Gadiel, Aziz Andambwile kiungo kutoka Mbeya City, mshambuliaji wa Mbeya Kwanza, Habib Kiyombo na beki wa Yanga, Paul Godfrey 'Boxer'.

## Mashindano ya Vishale Juni 24

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya mchezo wa Vishale yanatarajiwa kuanza Juni 24 hadi 26 mwaka huu, Kawe, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Vishale Tanzania ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Mchezo huo Afrika Mashariki, Victor Kimambo, alisema mashindano hayo hufanyika kila mwaka ambapo mwaka huu yatafanyika hapa nchini.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi za Kenya, Uganda, Rwanda pamoja na wenyeji Tanzania.

"Mashindano hayo yatashirikisha nchi pamoja na klabu zao, hivyo kila timu ya Taifa itakuja na klabu yake itakayoshirikisha wanawake na wanaume," alisema Kimambo.

Alisema maandalizi kwa upande wa Timu ya Taifa ambayo ina jumla ya wachezaji 6 yanasuasua kutokana na kukosa wafadhili licha ya kuanza kambi yao mapema Januari mwaka huu.

Alisema wametuma barua Baraza la Michezo Tanzania (BMT) kuomba msaada, lakini hadi sasa hawajapata jibu lolote.

## Lady Jaydee: Profesa Jay tuko pamoja

**Na Sabato Kasika**

IKIWA ni siku chache tangu rapa mkongwe Joseph Haule maarufu kama Profesa Jay atoke hospitalini, msanii mwenzake Judith Wambura 'Lady Jaydee', ameibuka na kuandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii kuwa 'Jay tunakuzimikiaaa'.

Jaydee ameonesha jinsia anavyomkubali rapa huyo, huku akimtaja Profesa Jay kuwa ni mmoja kati ya watu wake wa karibu, ambaye alisimama naye kwa nyakati zote hadi akafikia kuwa matawi ya juu.

Huku akiwa ameweka video kwenye ukurasa wake akisikiliza moja ya nyimbo za mkongwe huyo, Jaydee ameandika kuwa katika watu ambao akiulizwa na hatafikiria mara mbili kuwaunga mkono kwa lolote, ni Profesa Jay.

"Ni kaka pekee aliyesimama na mimi nyakati zote. Love you big bro. Tuko pamoja," aliandika Jaydee katika ukurasa wake wa mtandao ya kijamii, kuonyesha jinsi anavyomkubali mkongwe huyo.

Profesa Jay alilazwa hospitalini kwa takriban siku 127, lakini sasa ameruhusiwa kurudi nyumbani baada ya afya yake kuimarika, huku mke wake akitumia ukurasa wake wa mtandao kushukuru kwa kila aliyeshiriki kupambania afya ya mumewe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS AITAKA CITY

KIUNGO wa kati wa Leeds United na England, Kalvin Phillips, 26, ameiambia klabu hiyo anataka kuondoka msimu huu ili kujiunga na Manchester City. ***(Football Insider)***

### POGBA FRESH JUVENTUS

WAWAKILISHI wa kiungo wa kati wa zamani wa Manchester United, Paul Pogba, 29, wanakaribia kukamilisha mkataba wa miaka minne kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa kujiunga na Juventus kwa uhamisho wa bure. ***(Sky Sports)***

### BALE AGOMBEWA

TOTTENHAM Hotspur, Newcastle na Aston Villa ni miongoni mwa Klabu za Ligi Kuu England zinazomfuatilia mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, 32, ambaye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake na Real Madrid kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sun)***

### LUKAKU KUREJEA

CHELSEA wameanza mazungumzo juu ya kumwachia Romelu Lukaku, 29, kwenda Inter Milan kwa mkopo, lakini mshambuliaji huyo wa Ubelgiji atalazimika kukatwa mshahara. ***(Telegraph)***

### TARKOWSKI SAFI EVERTON

KLABU ya Everton imekamilisha usajili wa beki wa England, James Tarkowski, 29, kwa uhamisho huru kutoka Burnley, lakini mpango huo hautarajiwi kutangazwa hadi mwisho wa Juni. ***(Liverpool Echo)***

### VITINHA ATAKIWA MAN

MANCHESTER United wanapigiwa upatu kumsajili kiungo wa kati wa Porto na Ureno, Vitinha, 24, ambaye ana kipengele cha kuuzwa chenye thamani ya pauni milioni 34. ***(Abola)***

### KOUNDE AWINDWA

MATUMAINI ya Chelsea kumsajili mlinzi wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde, 23, hayatakoma licha ya mchezaji huyo kufanyiwa upasuaji wiki hii. ***(Standard)***

### ASENSIO ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL bado wanaweza kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Marco Asensio, 26, msimu huu huku mzozo kuhusu mshahara wake Real Madrid ukiendelea. ***(Sun)***

### BELLINGHAM AWANIWA

REAL Madrid wanatumaini kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, 18, licha ya ushindani kutoka kwa timu za Ligi kuu England, Manchester United na Liverpool kuhusu mkataba wa pauni milioni 78. ***(Metro)***

### BAZUNU KUTUA SOUTHAMPTON

KLABU ya Southampton imefikia makubaliano na Manchester City kumsajili kipa wa Ireland, Gavin Bazunu, 20. ***(90min).***

### FREDERICKS AGOMBEWA

KLABU ya Bournemouth inakaribia kumsajili beki wa West Ham, Ryan Fredericks, 29, lakini Fulham pia wanamtaka mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# PEREZ AMSHUKIA MBAPPE

**Adai wa sasa si yule aliyekuwa na ndoto ya kujiunga Real Madrid, kwani amebadilika sana...**

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez amesema Kylian Mbappe "lazima awe amebadilisha ndoto yake" baada ya mshambuliaji huyo wa Ufaransa kukataa kujiunga na klabu hiyo ya Hispania.

**Mbappe mwenye umri wa miaka 23, alitia saini mkataba mpya wa miaka mitatu na Paris St-Germain badala ya kuhamia klabu hiyo ya LaLiga.**

"Ndoto yake ilikuwa kucheza Real Madrid," alisema Perez akiiambia El Chiringuito.

"Tulitaka kufanya hivyo Agosti iliyopita na hawakumruhusu kuondoka, aliendelea kusema anataka kucheza Madrid na siku 15 kabla alibadilisha hali hiyo."

Kwa mujibu wa mchambuzi wa soka wa Hispania, Guillem Balague, Mbappe alishafikia makubaliano ya maslahi binafsi na Real Madrid miezi kadhaa iliyopita kabla ya kuamua kubakia PSG.

"Huyu sio Mbappe niliyetaka kumleta, ni mwingine, ambaye lazima atakuwa amebadilisha ndoto yake," alisema Perez akinukuliwa na gazeti la Marca kutoka kwenye mahojiano na El Chiringuito.

"Amebadilika, amepewa vitu vingine, amebanwa tayari.

"Hakuna mtu yupo juu ya klabu ndani ya Real Madrid. Ni mchezaji mkubwa, anaweza kushinda zaidi ya wengine, lakini ni mchezo wa pamoja na tuna maadili na kanuni ambazo hatuwezi kuzibadilisha."

Perez aliongeza: "Mbappe ambaye angekuja hapa sio huyu. Ikiwa ni hivyo, napendelea abaki PSG. Namtaka mwenye ndoto."

Real Madrid ilishinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita huku mshambuliaji wa Ufaransa Karim Benzema akifunga mabao 44 katika michezo 46.

Yeye ni mmoja wa wanaopewa nafasi kubwa ya kushinda Ballon d'Or na Perez alipendekeza uchezaji wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 uliokuwa nyuma yao kutomsajili mshambuliaji Erling Haaland, ambaye amejiunga na Manchester City.

"Tuna tisa bora zaidi duniani na hatukuweza kumleta Haaland ili kuwa naye kwenye benchi, sivyo?" alisema Perez.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,006,4

MECHI KALI
DUNDALK FC
VERSUS
SHAMROCK ROVERS
1 | 4.02
X | 3.43
2 | 1.79

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NUNEZ NI KAMA TORRES – KOCHA



**LIVERPOOL,** England

DARWIN Nunez ana sifa zinazofanana na za mshambuliaji wa zamani wa Liverpool, Fernando Torres, lakini anaweza kuwa na kasi zaidi, kwa mujibu wa mmoja wa makocha wa zamani wa Uruguay.

Uhamisho wa Nunez kutoka Benfica kwenda Liverpool ulithibitishwa Jumanne, huku klabu hiyo ya Ureno ikifichua kuwa wamemuuza kwa ada ya pauni milioni 64.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alifurahia msimu mzuri wa 2021-22, akitikisa nyavu mara 34 katika michezo 41 kwenye mashindano yote.

Torres, aliyeichezea Liverpool kati ya mwaka 2007 na 2011, alifunga mabao 81 katika mechi 142 akiwa na Wekundu hao kabla ya kufanya uhamisho wa fedha nyingi kwenda kwa wapinzani wao Chelsea, na katika kilele chake alichukuliwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani.


Na kocha msaidizi wa zamani wa Almeria, David Badia ambaye ni raia wa Uruguay amefanya ulinganisho kati ya Nunez na Torres, wenye kimo sawa.

Badia alifanya kazi na Nunez msimu wa 2019-20 katika ligi ya daraja la pili la Hispania, huku mshambuliaji huyo akifunga mabao 16 katika mechi 32 za ligi akiwa na Almeria kabla ya kuhamia Benfica.

Badia alisema kuhusu kumlinganisha na Torres: "Bila shaka, Fernando ni Mhispania, (hivyo) nitamlinda, lakini nadhani Darwin ana kasi kidogo kuliko yeye.

"Darwin anapokuwa na umiliki wa mpira, ni mchezaji mzuri sana, anaweza kuudhibiti mpira, anaulinda mpira.

"Labda Fernando (alikuwa) akifanya vitendo vile vile kwa kasi ya chini kidogo, hiyo pia ni nzuri kwa sababu unaweza kufanya mambo mengine mengi, lakini kwa maoni yangu, Darwin anaweza kufanya kwa haraka zaidi."



# Alves bai bai Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wamemjulisha Dani Alves kwamba, hatapewa mkataba mpya mara baada ya wa sasa utakapokamilika mwishoni mwa mwezi huu, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Hispania.

Alves alisajiliwa kwa muda mfupi baada ya mchezaji mwenzake wa zamani Xavi kurejea kama kocha na mkongwe huyo aliongezea matarajio kutokana na uchezaji wake, na kujiweka kuwa chaguo la kwanza la beki wa kulia wa Blaugrana hadi msimu uliomalizika.

Licha ya hayo, kumekuwa na sintofahamu juu ya kama Alves atapewa mkataba mpya msimu huu wa joto. Mkataba wake kwa sasa unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu na kwa mujibu wa Sport, klabu hiyo imefanya uamuzi, na kumfahamisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 kwamba hataendelea kuwepo.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa Alves alitamani sana kubaki na wababe hao wa Katalunya na hata kuashiria kuwa atakuwa tayari kusaini 'mkataba wa aina yoyote' ili kubakia.

Ingawa Barcelona bado wana matatizo ya kifedha wana mipango mikubwa ya usajili wa majira ya kiangazi.

## HABARI MICHEZO

442,235/-



# FAINALI ZFF KUPIGWA LEO

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

MCHEZO wa Fainali ya Kombe la ZFF (FA Cup) unatarajiwa kupigwa leo kwa kuzikutanisha Kipanga FC kutoka Unguja dhidi ya timu ya Chipukizi FC kutokea kisiwani Pemba.

Mchezo huo utachezwa katika uwanja wa Amaan majira ya saa 10:00 Alasiri huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita.

Bingwa wa FA ataiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, CAF.

**Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano, Ali Bakari "Cheupe" alisema matayarisho yote muhimu kuelekea mtanange huo yashakamilika kwa asilimia kubwa.**

Alisema tayari timu ya Chipukizi kutoka kisiwani Pemba imeshawasili hapa Unguja kwa mchezo huo ambao unazikutanisha timu ambazo hazijashiriki michuano ya kimataifa kwa muda mrefu.

Alisema kuwa ZFF kwa kushirikiana na Kamati ya Mashindano imeongeza zawadi ya fedha kwa mshindi wa pili tofauti na hapo awali ambapo bingwa pekee ndiyo aliyekuwa anapata zawadi ya Fedha.

Mshindi wa mchezo huo atajinyakulia kitita cha Shilingi Milioni 30 kutoka kwa Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ, na mshindi wa pili atapata shilingi milioni tano.



Mwimbaji wa muziki wa dansi, Christian Bella (kushoto), akitoa burudani katika hafla ya kukutanisha wazazi na watoto wao waliopoteana zaidi ya miaka 20 iliyopita, ambayo iliandaliwa na kituo cha redio cha Clouds FM kupitia kipindi cha Leo Tena jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TOC kufadhili wachezaji Olimpiki 2024

Na Shufaa Lyimo

KAMATI ya Olympic Tanzania (TOC) imetangaza ufadhili wa kimichezo kwa wachezaji watano ambao wanajiandaa na mashindano ya michezo ya Olimpiki yatakayofanyika mwaka 2024 jijini Paris nchini Ufaransa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa TOC, Filbert Bayi alisema, wanamichezo ambao wamepata ufadhili huo wanatoka kwenye mchezo wa kuogelea, riadha na judo.

Kuogelea itawakilishwa na muogeleaji, Hilal Hemed Hilal, wakati riadha ina wachezaji watatu ambao ni Gabriel Gerald, Alphonce Simbu na Failuna Mayanga.

Alisema kwa upande wa mchezo wa Judo nafasi hiyo amepata mchezaji mmoja ambaye ni Andrew Thomas Mlugu.

"Kamati ya Olympic imefanikiwa kuwapatia ufadhili wa kimichezo wachezaji wetu watano ambao wanajiandaa na mashindano ya Olympic kati ya wchezaji 16,watano tu ndio walifanikiwa kupata nafasi hii,"alisema Bayi.

Alisema gharama za ufadhili huo Kwa kila mchezaji ni Dola za Marekani 1,500 kwa mwezi (sawa na Shilingi 3,496,500), na kuongeza kuwa, ufadhili huo utadumu hadi mashindano hayo yatakapomalizika.

Naye Makamu wa Rais wa TOC, Henry Tandau aliwataka wanamichezo kuitumia vema fursa hiyo ili waweze kuliwakilisha vema Taifa katika mashindano ya Olimpiki.

"Hii ni fursa adimu kwa wanamichezo wetu, hivyo wajitume ili waweze kupata viwango vinavyotakiwa na hatimaye kuwa wachezaji bora jambo litakalowasaidia Kimataifa,"alisema.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/06/22 | 20:00 | Enppi Club vs Coca Cola | 3.47 | 2.92 | 2.28 |
| 02. 18/06/22 | 21:30 | Gimnasia Mendoza vs Deportivo Maipu | 2.28 | 2.78 | 3.68 |
| 03. 18/06/22 | 22:00 | Londrina PR vs Vasco da Gama | 3.26 | 2.86 | 2.42 |
| 04. 18/06/22 | 22:00 | Seattle Sounders vs Los Angeles FC | 2.30 | 3.53 | 2.97 |
| 05. 19/06/22 | 00:00 | Arsenal Sarandi vs Talleres | 2.60 | 3.10 | 2.90 |
| 06. 19/06/22 | 00:30 | Nautico PE vs Sport Recife | 2.73 | 2.97 | 2.73 |
| 07. 19/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Ceara CE | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 08. 19/06/22 | 01:10 | Almirante Brown vs Deportivo Moron | 2.44 | 2.76 | 3.36 |
| 09. 19/06/22 | 01:45 | Sportivo Ameliano vs Nacional Asuncion | 2.77 | 3.12 | 2.57 |
| 10. 19/06/22 | 02:30 | Sarmiento vs Patronato Parana | 2.58 | 3.18 | 2.88 |
| 11. 19/06/22 | 03:00 | Chicago Fire vs DC United | 2.21 | 3.43 | 3.22 |
| 12. 19/06/22 | 13:30 | Suwon Samsung vs FC Seoul | 2.69 | 3.09 | 2.74 |
| 13. 19/06/22 | 17:00 | Guarani SP vs CSA AL | 2.42 | 2.97 | 3.12 |
| 14. 19/06/22 | 19:00 | Jerv vs Ham-Kam | 2.88 | 3.33 | 2.39 |
| 15. 19/06/22 | 21:00 | Aalesunds vs Valerenga | 2.46 | 3.39 | 2.74 |
| 16. 19/06/22 | 21:00 | Gimnasia Jujuy vs Temperley | 2.33 | 2.72 | 3.66 |
| 17. 19/06/22 | 22:00 | Tenerife vs Girona | 2.44 | 3.08 | 3.03 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 17/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2755 | Pohang Steelers vs Gangwon | 1.82 | 3.32 | 4.01 |
| 13:45 | 5590 | Ffsa Ntc vs Salisbury Inter W | 3.73 | 4.22 | 1.68 |
| 14:30 | 4487 | Meizhou Kejia vs Beijing Guoan | 3.55 | 3.25 | 1.96 |
| 15:00 | 3858 | Boca Jrs vs CA Barracas Central Reserve | 1.34 | 4.70 | 7.05 |
| 16:00 | 4393 | Gasogi United vs Rayon Sports FC | 2.90 | 2.80 | 2.51 |
| 16:00 | 5784 | Etincelles vs Mukura | 2.43 | 2.74 | 3.09 |
| 17:30 | 1466 | FK Silas vs Kedainiai Nevezis | 2.54 | 3.42 | 2.41 |
| 18:00 | 1858 | FK Auda vs Spartaks Jurmala | 1.54 | 3.94 | 5.12 |
| 18:00 | 2824 | Lokomotiv Tashkent vs Sogdiyona Jizzax | 2.28 | 3.00 | 3.05 |
| 18:00 | 4224 | Belshina vs Energetik Bgu Minsk | 4.32 | 3.58 | 1.70 |
| 18:00 | 4270 | Banga Gargzdai vs FC Hegelmann Litauen Kaunas | 7.84 | 4.51 | 1.33 |
| 19:00 | 1138 | PPJ vs Peka | 2.06 | 3.58 | 2.99 |
| 19:00 | 1440 | Skeid Fotball 2 vs Ready | 1.44 | 4.91 | 4.91 |
| 19:00 | 1459 | Hammarby W vs Kopparbergs Go W | 3.54 | 3.49 | 1.89 |
| 19:00 | 3275 | Tampere United vs FC Ilves-Kissat | 2.21 | 3.92 | 2.55 |
| 19:00 | 3515 | Polonia Sroda Wlkp vs Pogon II Szczecin | 1.96 | 3.68 | 3.14 |
| 19:00 | 4809 | FS Metta/Lu vs BFC Daugavpils | 2.76 | 3.15 | 2.38 |
| 19:00 | 5086 | Volsungur vs Njarovik | 2.95 | 3.75 | 2.11 |
| 19:00 | 5114 | PK-35 Vantaa W vs Honka W | 1.54 | 4.42 | 4.42 |
| 20:00 | 1605 | Lidkopings FK vs IFK Kumla | 1.79 | 3.87 | 3.53 |
| 20:00 | 1644 | Hassleholms IF vs Kristianstads FF | 1.99 | 3.64 | 3.10 |
| 20:00 | 1977 | Vitebsk vs Torpedo Zhodino | 2.99 | 3.09 | 2.26 |
| 20:00 | 2387 | Bergnasets Aik vs Bodens BK | 14.72 | 7.66 | 1.11 |
| 20:00 | 2570 | FC Rosengaard vs FBK Balkan | 1.20 | 6.26 | 9.19 |
| 20:00 | 2617 | Qviding Fif vs Ljungskille | 3.93 | 4.03 | 1.67 |
| 20:00 | 3348 | Umeaa FC vs Piteaa IF | 1.58 | 3.83 | 4.82 |
| 20:00 | 3827 | Ceramica Cleopatra vs Farco FC | 2.24 | 2.87 | 3.58 |
| 20:00 | 3851 | ES Setif vs USM Alger | 2.27 | 3.03 | 3.03 |
| 20:00 | 4813 | Tolo IF vs Savedalens IF | 2.70 | 4.22 | 2.03 |
| 20:00 | 4923 | Ismaily SC vs Arab Contractors | 2.17 | 2.96 | 3.62 |
| 20:00 | 5083 | Fyllingsdalen vs Froya Fotball | 1.44 | 4.91 | 4.91 |
| 20:00 | 5187 | Stenungsunds IF vs Ahlafors IF | 3.57 | 4.30 | 1.70 |
| 20:00 | 5664 | Djerv 1919 vs Bremnes | 1.61 | 4.61 | 3.83 |
| 20:15 | 4804 | Vastra Frolunda IF vs Landvetter IS | 1.49 | 4.63 | 4.73 |
| 20:30 | 1406 | Trosa-Vagnharad SK vs Varmbols FC | 1.58 | 4.61 | 4.02 |
| 21:00 | 2712 | Villa Mitre vs CA Liniers Bahia Blanca | 1.69 | 3.45 | 5.20 |
| 21:00 | 4890 | Sportivo Dock Sud vs Ituzaingo | 2.66 | 2.76 | 2.76 |
| 21:30 | 2048 | Defensores Unidos vs Canuelas | 1.91 | 2.99 | 4.12 |
| 21:30 | 3430 | Boca Unidos vs Gimnasia Y Tiro De Salta | 3.78 | 3.00 | 1.99 |
| 21:30 | 3641 | Sarmiento Resistencia vs Def Belgrano VR | 1.82 | 3.04 | 4.51 |
| 21:30 | 4367 | B71 Sandoy vs Vikingur Gota II | 2.09 | 4.33 | 2.56 |
| 21:45 | 1681 | Cobh Ramblers vs Wexford Youths | 3.04 | 3.53 | 2.05 |
| 21:45 | 1709 | Dundalk FC vs Shamrock Rovers | 4.02 | 3.43 | 1.79 |
| 21:45 | 1772 | Bohemians FC vs Shelbourne | 1.88 | 3.08 | 4.11 |
| 21:45 | 2691 | Derry City vs Drogheda Utd | 1.25 | 5.13 | 9.28 |
| 21:45 | 3220 | Bray Wanderers vs Galway United | 4.53 | 3.64 | 1.65 |
| 21:45 | 4073 | Juventud Unida G vs Union Sunchales | 4.80 | 2.94 | 1.81 |
| 21:45 | 4378 | Treaty United vs Athlone Town | 1.57 | 4.02 | 4.70 |
| 21:45 | 4975 | St Patricks vs UCD Dublin | 1.35 | 4.50 | 7.25 |
| 22:30 | 4887 | Talaea El Gaish vs Smouha Club | 2.86 | 2.71 | 2.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Juni 17, 2022

Nipashe



Perez amshukia Mbappe UKURASA 21




Mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga. **PICHA: YANGA**

## Simba SC yadai Phiri alikataa ofa ya Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kuwa mara kadhaa straika, Moses Phiri alikataa ofa ya klabu ya Yanga ambao walitaka kumsajili.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema jana kuwa viongozi wa klabu hiyo walisafiri mara kadhaa kwenda nchini Zambia kumshawishi kujiunga na timu yao, lakini Phiri ni mchezaji mwenye malengo makubwa akakataa ofa hizo.

Alikuwa akizungumza baada ya klabu ya Simba juzi usiku kumtambulisha rasmi Phiri, straika aliyesajiliwa kutokea Zanaco ya Zambia.

"Ni kweli wamesafiri mara kadhaa kwenda kumshawishi, lakini mchezaji mwenye malengo makubwa Afrika hii ni lazima aichague Simba. Haikuwa ngumu sana kwa upande wetu kwa sababu tuna faida ya kuwa timu kubwa kwa sasa, mchezaji mwenye kiu ya mafanikio akipelekewa ofa mbili kutoka Tanzania, basi chaguo lake la kwanza itakuwa ni Simba. "Utakumbuka hata huko nyuma alikuwa akijiposti akiwa amevaa jezi ya Simba, yeye ndiye alikuwa akimuomba Clatous Chama amletee jezi," alisema Ahmed.

Kuhusu usajili wake alisema kuwa tayari umekamilika na amesaini mkataba wa miaka miwili na alitarajiwa kuwa sehemu ya watazamaji jana kwenye mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Tayari tumeanza harakati za usajili kama tulivyowaahidi kuwa tunawashusha watu wa maana, watu wa kuja kuisaidia Simba, watu wa kuifanya Simba kuchanua makucha yake, na uzuri ni kwamba watu wengi wa Afrika Mashariki na Kusini wanamfahamu vizuri mchezaji huyu," alisema.

Juzi kwenye mtandao rasmi wa instagram, Simba ilitangaza rasmi kumsajili mchezaji huyo, baada ya tetesi za muda mrefu kuwa ilishaingia makubaliano naye ya awali tangu kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Ilidaiwa kuwa awali Simba ilitaka kumsajili kipindi hicho, lakini klabu yake ya Zanaco ilikataa kumtoa kwa sababu tayari ilikuwa imeshaingia kwenye hatua za makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wakati huo huo, klabu ya Simba imeipongeza Yanga kwa kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu.

Kwenye mtandao wao wa instagram iliandika "Tunawapongeza Yanga kwa kutwaa Ubingwa wa Ligi Kuu 2021/22.

# Nabi atoa ubingwa kwa familia

### ●●● Asema haikuwa kazi rahisi, asifia usajili wa Sure Boy kuleta chachu...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA mkuu wa mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania bara, Yanga, Mohamed Nasreddine Nabi amesema ubingwa huo ni zawadi kwa familia yake ambayo imekuwa ikimfariji mara kwa mara licha ya kuwa mbali nayo.

**Yanga juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Coastal Union na kutangazwa kuwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania bara baada ya kufikisha pointi 67 ambazo hazitafikiwa na timu nyingine yoyote, ikiwa imecheza mechi 27 zikibaki tatu.**

Mabao ya Yanga yakifungwa na Fiston Mayele aliyetikisa nyavu mara mbili na Ushindi Chiko, mchezo ukipigwa uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Nabi alisema ilikuwa safari ndefu hadi kufanikiwa kutwaa Kombe hilo.

"Nimefurahi kupata ubingwa, haikuwa kazi rahisi nawapongeza wachezaji wangu pamoja na Uongozi wa Yanga kwa ushirikiano walionionesha hadi leo (juzi) tumefanikiwa kupata ubingwa," alisema Nabi.

Alisema mechi zote ambazo wamecheza zilikuwa ni kama fainali na kudai kila timu ambayo walicheza nayo ilikuwa inawakamia kwa kiasi kikubwa, lakini walikuwa hawawapi nafasi.

Alisema watauendeleza ushindani huo kwenye michezo mitatu iliyobakia ili wamalize msimu huu wakiwa hawajapoteza mchezo hata mmoja.

Akizungumzia mchezo wenyewe, Nabi alisema kipindi cha kwanza kilikuwa kigumu kwao kwani Coastal Union walikuwa wapelekesha kwa presha kubwa.

Alisema aliwaita wachezaji wake na kuwaambia kwamba, wanatakiwa kutojikaba ili kupata nafasi na hatimaye kipindi cha pili walifanikiwa kutawala mchezo na kupata ushindi huo.

Wakati huo huo, Nabi alimsifia kiungo Salum Abubakar 'Sure Boy' kuwa ni usajili ambao ameupenda kwa sababu ni mchezaji alioyeongeza nguvu ndani ya kikosi cha timu hiyo licha ya nyota huyo kuhitaji kuongezewa vitu kidogo ili kuwa bora zaidi.

"Sure Boy ni moja ya usajili mzuri ambao Yanga walifanya, ameleta nguzu ndani ya kikosi na amesaidia sana safu ya kiungo," alisema Nabi kuhusu nyota huyo wa zamani wa Azam FC.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042